# Nipashe

MWANGA WA JAMII

Jumanne Septemba 10, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581795

www.ippmedia.com

The Guardian digital

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US




UKURASA 22

**RONALDO APIGA BAO LAKE LA 901**

**Ugomvi** mume na mke wasababisha kifo cha kichanga wa miezi saba

UKURASA 5

**Mpango:** Kila mwaka hekta 24,151 za misitu zinateketea

UKURASA 3



**Wanaharakati** wawatetea wanaojaribu kujitoa uhai, wasiadhibiwe

UKURASA 3

## MAZIKO KADA CHADEMA

UKURASA 2

# Masauni katika wakati mgumu



"Tumesikitishwa sana na kuhuzunishwa na kusononeshwa, ni jambo ambalo halikupaswa kutokea katika nchi yetu"



"Uongozi wa Wizara ya Mambo ya Ndani katika ngazi zote ujitafakari iwapo unastahili kuendelea kuwapo wakati tuhuma hizi nzito za watu kutekwa zikiendelea kusikika sehemu mbalimbali

**Deodatus Balile**



"Mnaofanya hayo, iwe kwa sababu yoyote ile, mjue yupo Mungu, nasi tunamwomba adhihirishe wazi uwezo na mamlaka yake, Mungu hadhihakiwi"

**Askofu Dk. Fredrick Shoo**




"Rais Samia aunde tume ya kimahakama kuchunguza utekaji, utesaji na mauaji yanayoendelea kumea nchini"

**Freeman Mbowe**

"Mauaji na kupotea kwa watu pamoja na kukamatwa, kupigwa na juhudi nyingine za kuwaengua raia katika uchaguzi, havipaswi kuwa na nafasi katika demokrasia".

**Ubalozi wa Marekani**





Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe (kushoto) akiwa amebeba jeneza lenye mwili wa aliyekuwa kada wa chama hicho, Ally Kibao wakati wa maziko yaliyofanyika jijini Tanga jana. **PICHA: CHADEMA**

## Wasio na vyoo waondolewa vituo vya maboresho Daftari la Wapigakura

UKURASA 4

**MICHEZO** **MOROCCO ATAJA MBINU STARS KUIUA GUINEA** UK.24 **MAONI,** UK.6

# Waziri Masauni katika wakati mgumu

**Na Jenifer Gilla**



Wakazi wa jijini Tanga wakiwa kwenye maziko ya kada wa Chadema, Ally Kibao jana.
**PICHA: CHADEMA**

HAMAD Masauni yuko katika wakati mgumu, akishinikizwa kujiuzulu cheo chake cha Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kutokana na matukio ya mauaji, utesaji na utekaji yanayoendelea nchini.

Kukiwa na shinikizo hilo, Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kimemwomba Rais Samia Suluhu Hassan kuunda tume ya kimahakama kuchunguza matukio ya watu kutekwa, kuteswa na kuuawa yanayoendelea kuripotiwa nchini.

Shinikizo la Waziri Masauni kuachia ngazi lilikolea zaidi jana wakati wa mazishi ya Ally Kibao, Mjumbe wa Sekretarieti ya CHADEMA na Msaidizi wa Katibu Mkuu wa chama hicho yaliyofanyika nyumbani kwake, Sahare, mjini Tanga na maziko yake kufanywa katika Kijiji cha Tarigube, Kata ya Togoni saa tisa alasiri.

Kibao anadaiwa kuwa jioni ya Septemba 6 mwaka huu, maeneo ya Kibo Complex Tegeta, Dar es Salaam, akiwa safarini kuelekea nyumbani kwake Sahare, Tanga na basi la Tashrif, alishushwa na watu waliokuwa na bunduki.

Asubuhi ya Jumamosi iliyopita, mwili wake ulikutwa maeneo ya Ununio, Tegeta ukiwa na majeraha makubwa, ikiwamo usoni.

Akiwa kwenye msiba huo jana, Mwenyekiti wa CHADEMA Taifa, Freeman Mbowe, alimwomba Rais Samia aunde tume ya kimahakama ili ichunguze matukio ya utekaji, utesaji na mauaji yanayoendelea kwa kuwa yeye pekee ndiye mwenye mamlaka hayo.

Alisema chama hicho kinaamini kuwa njia hiyo ndiyo pekee inayoweza kusaidia ili hata wale wenye ushahidi ambao hawawezi kuutoa kwa polisi, watautoa kwa tume hiyo.

Alidai kuwa baadhi ya watu wanaotekeleza vitendo hivyo, serikali inawafahamu kwa kuwa alishawahi kutaja baadhi ya majina katika mkutano na waandishi wa habari, lakini hakuna hatua zilizochukuliwa.

Alisema hakubaliani na kauli ya Rais kuelekeza Jeshi la Polisi kuchunguza suala hilo ilhali lenyewe ndio watuhumiwa namba moja wa chama hicho.

"Leo mnaweza kuona kuwa amani hii inayumba katika msiba huu, kuna siku amani hii msipoangalia itayumba katika mitaa yote ya nchi hii," alionya.

Mbowe alisema kuna Watanzania wengi wanapotea, wakijumuisha waojihusisha na wasiojihusisha na siasa, hali kadhalika wafanyabiashara.

"Tume ya kijaji ya kimahakama ndio chombo pekee kinachoweza kuyahoji makundi yote kikamshauri Rais hatua za kuchukua na kuwabaini wahalifu," alisema.

Alidai kuwa ndani ya vyombo vya ulinzi na usalama, mna watu wema, lakini miongoni mwao, wamo pia watu ambao ni wahalifu wa kutisha.

**VURUGU MSIBANI**

Wakati Waziri Masauni anaanza kuwasilisha salamu za pole kwa dua ya kumwombea marehemu, baadhi ya waombolezaji walisikika wakimzomea na kumtaka asiendelee, huku wengine wakisema, "Masauni jiuzulu... Masauni aondoke..."

Ni hali iliyomlazimu Mwenyekiti Mbowe kuingilia kati na kuwasisitiza watu hao watulie ili amalizie hotuba yake ili mambo mengine yaendelee.

"Ninataka kutoa rai kwa wana CHADEMA, tusiwe sababu ya kuvuruga msiba huu, ajenda yetu tunayoidai tutaendelea kuidai, lakini lazima turuhusu msiba huu uendelee kwa utulivu," alisema.

Akiendelea na hotuba hiyo, Masauni alisema serikali na Rais Samia wamesikitishwa na tukio hilo na kuagiza uchunguzi ufanyike haraka ili wote waliohusika wafikishwe kwenye vyombo vya sheria.

Aliwahakikishia waombolezaji kuwa serikali haitoliacha suala hilo "liende hivi hivi" na maelekezo ya Rais yameshaanza kufuatwa na hatua zitachukuliwa kwa watakaobainika.

"Tumesikitishwa sana na kuhuzunishwa na kusononeshwa, ni jambo ambalo halikupaswa kutokea hasa katika nchi yetu ambayo miaka yote tumekuwa tukijivunia usalama na amani kulinganisha na nchi nyingine zinazotuzunguka," alisema.

Mwenyekiti CHADEMA Kanda ya Kaskazini, Godbless Lema alisema alitegemea waziri huyo pamoja na Mkuu wa Jeshi la Polisi Camilus Wambura kujiuzulu kufuatia kuendelea kuwapo kwa matukio hayo ya kinyama.

"Mheshimiwa Waziri nikuombe sana, usiende tena kwenye msiba wa mtu aliyetekwa, nenda kwenye msiba wa mtu aliyeuawa bila kutekwa, mnatumiza, Nilitegemea baada ya kauli ya Rais jana (juzi), wewe leo (jana) uwe umejiuzulu, IGP awe amejiuzulu na viongozi wengine wakae kando," alisema.

Lema alisema kuwa aliposikia taarifa za kukamatwa kwa kada huyo, alihisi kuwa ni jambo la kawaida na angeachiwa baada ya muda mfupi, lakini taarifa za kifo ziliumiza moyo wake.

Alimweleza Waziri Masauni kuwa jana alipokea ujumbe katika simu yake, unaompa angalizo kuwa kama mwezi huu utaisha bila yeye na aliyekuwa Meya wa Manispaa ya Ubungo, Boniface Jacob, kutekwa na kuuawa, basi wamshukuru Mungu.

Alishauri serikali kutoruhusu mambo hayo kuendelea kufanywa nchini kwa kuwa maisha ya wanasiasa yamekuwa magumu, wakitembea na wasiwasi kuwa muda wowote wanaweza kutekwa na kuuawa na kuziacha familia zao.

Aliwashauri wananchi kushikamana na kukemea jambo hilo kwa pamoja badala ya kuachia CHADEMA pekee yake kwa kuwa yakiachiwa, hata wahuni wanaweza kuendeleza vitendo hivyo wakijua kuwa hayajaliwi na serikali.

Katibu Mkuu wa CHADEMA, John Mnyika, alimweleza Waziri Masauni kuwa anaunga mkono kauli za viongozi waliojitokeza kuhoji uwajibikaji wake kwa sababu matendo hayo yanatokea katika wizara ambayo anaongoza na hakuna kinachofanyika kuyakomesha.

Alisema kuwa Kibao hakuwa maarufu, lakini alikuwa na uwezo mkubwa wa kitaalamu katika kazi, akisisitiza "ndio sababu ya kutekwa na kuuawa", akivinyooshea kidole vyombo vya dola kwa madai kuwa huenda vimehusika.

Makamu Mwenyekiti wa Chama cha ACT Wazalendo Bara, Isihaka Mchinjita, alisema matukio kama hayo yanazusha hofu kwa wananchi kuhusu usalama wao na kumshinikiza waziri huyo ajiuzulu kwa kushindwa kuyadhibiti.

Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Balozi Batilda Burian, alisema amesikitishwa na msiba huo na kuwataka wananchi wa mkoa huo kumwombea kwa Mwenyezi Mungu Kibao ili ampokee na amsamehe dhambi zake.

Mjumbe wa Kamati Kuu Taifa wa Chama cha Tanzania Labour Party (TLP), Wilson Elias, alitaka serikali kukaa pamoja na vyama vya siasa nchini ili kutafuta suluhisho la kukomesha vitendo hivyo kabla havijaamua kuomba msaada kimataifa.

Alisema matukio hayo ya kutisha yanayolenga zaidi wanasiasa kutoka vyama vya upinzani, hayawakatishi tamaa wala kuwarudisha nyuma katika harakati zao za kutetea maslahi ya Watanzania.

**CCT YAKEMEA**

Jumuiya ya Kikristo Tanzania (CCT) pia imelaani vikali tukio la kuuawa kwa kada huyo wa CHADEMA na kusisitiza kuwa matukio ya utekaji na mauaji yafike mwisho kwa kuwa yanaumiza jamii ya Watanzania.

Askofu Mkuu wa Dayosisi ya Kaskazini ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzani (KKKT) na Mwenyekiti wa jumuiya hiyo, Dk. Fredrick Shoo alisema wamesikitishwa na mauaji na ukatili wanaofanyiwa Watanzania wasio na hatia.

"Mnaofanya hayo, iwe kwa sababu yoyote ile, mjue yupo Mungu, nasi tunamwomba adhihirishe wazi uwezo na mamlaka yake, Mungu hadhihakiwi," alisema.

Askofu Dk. Shoo alitoa wito kwa Watanzania waombe kwa dhati na kukemea vitendo hivyo vinavyotaka kutishia usalama, haki na amani ya nchi.

Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF) limeunga mkono hoja ya CHADEMA kumwomba Rais kuunda tume ya majaji kuchunguza wimbi la utekaji na mauaji, ambalo lilianza kwa mtu mmoja mmoja sehemu mbalimbali nchini.

Taarifa iliyotolewa jana na Mwenyekiti wa Jukwaa hilo, Deodatus Balile ilieleza kuwa matukio hayo yalianza kwa watoto na sasa watu wazima wanashushwa katika magari ya abiria na kuuawa.

TEF pia imeutaka uongozi wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi katika ngazi zote, ujitafakari iwapo unastahili kuendelea kuwapo wakati tuhuma hizi nzito za watu kutekwa zikiendelea kusikika sehemu mbalimbali nchini pamoja na kuwekwa wazi majina ya wanaofanya uchunguzi huo.

Ubalozi wa Marekani nchini pia umetoa wito kufanyika uchunguzi huru na uwazi na haraka kuhusu utekaji unaoendelea na mauaji ya Kibao kwa kuwa matukio hayo hayapaswi kupewa nafasi katika demokrasia ya Tanzania.

"Mauaji na kupotea kwa watu pamoja na kukamatwa, kupigwa na juhudi nyingine za kuwaengua raia katika uchaguzi zilizotokea mwezi uliopita, havipaswi kuwa na nafasi katika demokrasia," inasomeka sehemu ya taarifa hiyo ya Ubalozi wa Marekani nchini.

Vilevile, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora imelaani tukio la mauaji ya kada huyo CHADEMA, ikisisitiza inaendelea na uchunguzi wa tukio hilo.

Mwenyekiti wa Tume hiyo, Jaji mstaafu Mathew Mwaimu alisema wanatambua tamko la Rais Samia, lakini wao kama tume, wanaendelea na uchunguzi na baadaye watatoa tamko lao.

Alisema tume hiyo pia inaendelea na uchunguzi wa matukio mengine ya kikatili yanayofanywa na watu wasiojulikana nchini na kukatisha uhai wa watu, akisisitiza vitendo hivyo havikubaliki mbele ya jamii.

# Wapendekeza wanaojaribu kujiua kuondolewa adhabu

**Na Christina Mwakangale**

WATETEZI haki na afya ya binadamu wamependekeza kuondolewa kwa sheria ya adhabu kwa watu wanaojaribu kujiua.

Badala yake wamependekeza kuwapo kwa wigo wa uponyaji kisaikolojia na usaidizi wa afya ya akili.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Michelle Chapa Foundation, Dk. Michelle Chapa, alisema hayo wakati wa kampeni ya kuondoa Sheria ya Adhabu ya Kujiua nchini, katika mada iliyoendeshwa mtandaoni, iliyoandaliwa na Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe.

Dk. Michelle alisema kuondolewa kwa sheria hiyo kutabadilisha mazungumzo kuhusu kitendo hicho, kwa kuondoa lawama kwa wanaotenda matukio hayo kwa kuwa wengi wao sababu kuu ni kuzongwa na magonjwa ya akili.

Kwa mujibu wa kifungu cha 217 cha Kanuni ya Adhabu Sura ya 16, kujaribu kujiua ni kosa la jinai; linaweza kuhukumiwa kwa adhabu isiyozidi miaka mitano jela, kama inavyoelekezwa na kifungu cha 35 kinachoeleza adhabu ya jumla kwa makosa ambayo hayajapewa adhabu ya moja kwa moja.

Pia, sheria hiyo inaweka kinga katika kifungu cha 13 na inatoa msamaha kwa watu wanaofanya makosa wakiwa katika hali ya ugonjwa unaoathiri akili zao na kufanya wasielewe wanachofanya.

Dk. Michelle, alisema lengo la mada hiyo ni kukuza uelewa kuelekea maadhimisho ya Siku ya Kujizuia Kujiua Duniani, inayofanyika Septemba 10, kila mwaka.

Alisema matukio ya aina hiyo huwa hayazungumziwi sana katika jamii na kuna sababu nyingi, ikiwamo mila, unyanyapaa na kwamba wadau mbalimbali kama vile Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe (MNMH), wamemekuwa wakiiadhimisha siku hiyo, kwa kuwapo makongamano.

Mwanasheria Jebra Kambole, alisema kesi za aina hiyo zipo na tayari huwa zimefikishwa katika mahakama na kwamba adhabu hiyo imeendelea kutekelezwa nchini kutokana na kurithiwa kutoka kwa wakoloni, ambao kwa sasa hata wao hawaitumii tena.

Alisema ni vyema jamii ikaelewa kwamba kukaribia kufanya kosa hilo ni jinai, hivyo mapendekezo ni kwamba mtu aliyejaribu huhitaji tiba kiafya na ndiyo sababu ya wadau kuhamasisha kuondolewa kwa adhabu hiyo.

Alisema: "Ni kosa la kikoloni na wao walishaliondoa kwao, sisi bado tumeikumbatia, watu wanaojaribu kufanya kosa hilo wanahitaji tiba ya kisaikolojia, kwa sababu hata akifungwa ile nia yake atakuwa nayo.

Zamani pia katika familia ikitokea mtu kafanya kosa hilo, aliadhibiwa kwa kutengwa."

# Mpango ahadharisha hali ya mazingira ni mbaya

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, (pichani) amesema hali ya mazingira nchini ni mbaya na wastani wa hekta 24,151 za misitu zinazopotea kila mwaka huku akitaja sababu kadhaa ikiwamo inayotuhumu baadhi ya wafanyabiashara wa mkaa kuwa ni watoa maamuzi na wana maslahi binafsi.



Akizungumza jana kwenye mkutano maalum wa viongozi, wataalamu na wadau wa mazingira kuhusu hali ya mazingira nchini, Dk. Mpango alisema: "Tanzania inalia, athari za uharibifu wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi ni kubwa sana zimetuathiri kwa kiasi kikubwa sana, zinahatarisha uhai wa viumbe vyote ikiwamo sisi wanadamu, usalama wa chakula, upatikanaji wa maji na magonjwa ya mlipuko."

Alisema taarifa ya nne ya mazingira ya mwaka 2024 inaonesha hali ya utunzaji na uhifadhi wa mazingira nchini haliridhishi.

"Nchi yetu inakabiliwa na changamoto mbalimbali za mazingira ambazo kwa kiasi kikubwa zinatokana na tabia ya watu, ukataji ovyo wa miti na uharibifu wa misitu ambapo takwimu zinaonesha ongezeko kubwa la uharibifu wa misitu kutoka hekta 372,816 kwa mwaka 2019 hadi 469,420 kwa mwaka 2023," alisema.

Alisema wastani wa hekta 24,151 zinazopotea kila mwaka na uharibifu huo unachangiwa kwa sehemu kubwa na shughuli za binadamu zisizo endelevu ikiwamo utegemezi mkubwa wa nishati ya kuni na mkaa.

Kadhalika, alisema takwimu zinaonesha kuwa tani milioni saba za taka ngumu zinazalishwa nchini kila mwaka ambapo wastani wa tani milioni 3.5 ndio zinazokusanywa na kutupwa maeneo yanayostahili na zilizobaki hutupwa ovyo.

"Katika matumizi ya nishati chafu, takwimu za sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022, asilimia 82 za nishati inayotumika kwa ajili ya kupikia inatokana na kuni na mkaa, matumizi ya nishati chafu inasababisha ukataji wa miti ili kukidhi mahitaji makubwa ya nishati ya kupikia," alisema.

Alisema moja ya sababu zinazochangia hali ya mazingira kutokuwa nzuri ni pamoja na uwapo wa sheria kinzani na kutolea mfano sheria iliyounda Wakala wa Misitu (TFS) bado inafanya mkaa kuwa chanzo cha mapato na inahamasisha utoaji wa vibali vya kukata miti ili kutengeneza mkaa.

Alisema anachoona ni kasi ya ukataji miti isiyoendana na kasi ya upandaji miti, bado elimu kwa umma haitoshi ikiwamo kubadili mazoea kwenye kilimo.

"Badala ya kulima kwa kuchoma moto kuandaa mashamba, lakini bado wananchi wetu hawatusikii, kwa hiyo pengine nafikiri namna yetu ya kutoa elimu kwa umma haiendi kwa namna ambayo watu wetu wanaelewa, tunahitaji kujitazama vizuri, tutumie mbinu gani ili elimu hii iwafikie wananchi wetu," alisema.

"Wenye kipato kidogo wanashindwa kumudu teknolojia za kijani za nishati safi ya kupikia na serikali ina uwezo mdogo wa kutoa ruzuku, hizi changamoto naamini kupitia mkutano huu itazijadili na kuja na mapendekezo ya namna ya kwenda mbele ili Tanzania iache kulia kutokana na uharibifu wa mazingira."

Alitaka mkutano huo uainishe namna bora ya kufikia matokeo tarajiwa kwa kutafuta majibu ya changamoto za kimazingira zilizopo ikiwamo usimamizi wa mazingira nchini.

Alimwagiza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Muungano na Mazingira, Dk. Ashatu Kijaji, kuwasilisha kwake taarifa ya mkutano huo na mapendekezo yatakayotolewa mapema iwezekanavyo.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Dk. Ashatu Kijaji, alisema kupitia mkutano huo mada nane zitajadiliwa ikiwamo ya biashara ya kaboni na inatarajiwa kuongeza hamasa ya uwajibikaji katika kukabiliana na uharibifu wa mazingira nchini.

Awali, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Zanzibar, Harusi Said Suleiman, alisema Zanzibar imeathiriwa na mabadiliko ya tabianchi kwenye mazingira na Agosti 17, mwaka huu walizindua programu ya kuirudisha Zanzibar ya kijani.


**SHASHINHALE AUCTION MART & COURT BROCKERS LIMITED**
(Dealers in: Court Broker, Debt Collectors, and Commission Agent, Legal consultant)
P.O BOX 288, GEITA. **TANZANIA.**

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kwa Idhini tuliyopewa na Azania Bank,tunatoa notisi ya siku 14 kuanzia tarehe ya tangazo hili kwa mdaiwa anaetajwa hapo chini alipe deni analodaiwa na Benki hiyo pamoja na riba,kushindwa kulipa kwa mda huo,tutalazimika kuuza dhamana iliyowekwa kwa njia ya Mnada wa hadhara kulingana na Tarehe zilizowekwa, mda ni kuanzia saa **4:00 Asubuhi** nakuendelea.

| Na. | JINA LA MDAIWA/MDHAMINI | MAELEZO YA DHAMANA NA MAHALI ILIPO | TAREHE YA MNDA |
|---|---|---|---|
| 1 | KAYANDA NYALIKA | HOTEL ILIYOPO MTAA WA MWATULOLE GEITA MJINI KIWANJA NA.13 KITALU "G" | 25/09/2024 |
| 2 | JOHNSON NICOLAUS MAHAGULA/JONHSON JACKSON NA PIUS CO LTD | NYUMBA YA MAKAZI IPO MTAA WA KAGERERA B,KIWANJA NA.244 KITALU "E" YENYE UMILIKI UNAOSOMEKA JONHSON NICOLAUS MAHAGULA | 26/09/2024 |
| 3 | GHATI JOSEPH CHACHA | NYUMBA YA BIASHARA ILIYOPO MTAA WA MWATULOLE,KIWANJA NA.169 NA 170 KITALU "C" GEITA MJINI | 25/09/2024 |
| 4 | PASCAL PETRO MUGABE/MILEM INVESTMENT CO LTD | NYUMBA YA BIASHARA KIWANJA NA.90 KITALU "E" GEITA MNJINI UMILIKI UNASOMA PASCAL PETRO MGABE.NYUMBA IPO KARIBU NA UWANJA WA KALANGALALA | 27/09/2024 |
| 5 | MARY LEONARD RUSHITA | NYUMBA YA MAKAZI ILIYOPO MTAA WA MWATULOLE KIWANJA NA.132 KITALU "F" GEITA MJINI. | 27/09/2024 |
| 6 | ANDREW JOHN SHIRIMA/ANSI TIMBER GENERAL SUPPLIES LTD | NYUMBA YA MAKAZI ILIYOPO MTAA WA NYAMALEMBO,KIWANJA NA.77 KITALU,GEITA MJINI YENYE UMILIKI UNAOSOMEKA ANDREW JOHN SHIRIMA. | 26/09/2024 |
| 7 | SAMWEL LUCAS MAGUHA | NYUMBA YA BIASHARA ILIYOPO PASIANSI MWANZA KIWANJA NA.1114,KITALU "M" | 7/10/24 |
| | | NYUMBA YA BIASHARA ILIYOPO ILEMELA MWANZA KIWANJA NA.17 KITALU "A" | 8/10/24 |
| | | NYUMBA YA BIASHARA ILIYOPO KAHAMA MJINI KIWANJA NA.446 KITALU "A" | 30/09/2024 |
| | | NYUMBA YA MAKAZI ILIYOPO IGUDIJA-KATA YA BUGHARAMA,WILAYA YA MSALALA. | 15/10/2024 |

**MASHARTI YA MNADA.**

1. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
2. Mnunuzi atapaswa kulipa 25% ya bei iliyofikiwa siku ya mnada
3. Malipo ya 75% yanatakiwa kulipwa ndani ya siku 14,kushindwa kufanya hivyo 25% haitorudishwa.
4. Gharama za Kuhamisha umiliki,Kumwondoa aliepo ndani ya Nyumba Mdaiwa/Mpangaji zipo juu ya Mnunuzi.

**Kwataarifa Zaidi wasiliana na,**
**Mkurugenzi Mtendaji,Shashinhale Auction Mart**
**Barabara ya Bomani Mahakamani, Geita Mjini**
**0657824547/0757006076.**

**Au**

**Azania Bank,**
**Mawasiliano Towers,Head Office,**
**S.l.p 32089 Dar es salaam,**
**255 222412025/6/7**

# Wadaiwa kuondolewa vituo vya maboresho ya Daftari la Wapigakura

**Na Vitus Audax**

BAADHI ya wananchi katika Kata ya Mwandoya, Jimbo la Kisesa, wilayani Meatu, mkoani Simiyu wamedai kuondolewa katika vituo vya kujiandisha na kuboresha taarifa za Daftari la Kudumu la Mpigakura.

Wanadai hatua hiyo ni sehemu ya operesheni ya kutekeleza uchimbaji vyoo kwa kila kaya ili kukabiliana na ugonjwa wa kipindupindu.

Hata hivyo, hatua hiyo inatajwa kuingilia na kukwaza maboresho ya daftari hilo yalioanza Septemba 3 mwaka huu, yakitarajiwa kuhitimishwa leo Septemba 10, hali inayodaiwa kusababisha wananchi kukimbia makazi yao, msako ukifanywa na mgambo kwa kushirikiana na Idara ya Afya.

Mwenezi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Kata ya Mwandoya, Luhende Gamanija alisema msako huo ulianza Septemba 8 wakati maboresho ya daftari hilo yakielekea ukingoni na kuwa watu walianza kutafutwa kwenye makazi na maeneo wanakojiandisha na kupigwa faini huku wengine wakichukuliwa kwenda kuchimba vyoo. "Hivi karibuni kuliripotiwa mlipuko wa ugonjwa wa kuhara na kutapika katika maeneo yetu, hivyo kuhusishwa na kipindupindu kutokana na watu wengi kutokuwa na vyoo, hivyo hujisaidia vichakani.

"Lakini hakukuwa na operesheni ya namna hii, juzi tu wakati tunaendelea na maboresho wameanzisha opereshini ya kuchukua watu wakachimbe vyoo kwenye makazi yao huku wengine wanaokutwa hawana vyoo wakitozwa faini kuanzia Sh. 50,000 hadi 300,00 ambazo hazitolewi risiti," alisema.


Alisema kuwa kufuatia hatua hiyo, watu wamekimbia makazi yao na kuacha shughuli za kujiandisha, akiwaomba viongozi kuingilia kati suala hilo ili kutokupoteza haki za watu kushiriki kikamilifu katika uchaguzi.

Akizungumza na Nipashe, Mbunge wa Kisesa Luhaga Mpina, alithibitisha kupokea taarifa hizo na kueleza kuwa, kwa wakati huo alikuwa safarini, hivyo kulazimika kurejea jimboni kuona namna ya kumaliza tatizo hilo. "Kwa sasa namtafuta Mkuu wa Wilaya ili tujue namna ya kulifanyia kazi na wakati huu ninaelekea jimboni, tunaendelea kuwasiliana ili kama kuna operesheni isitishwe, tuendelee na maboresho ya daftari la kudumu la mpigakura," alisema Mpina.

Mratibu wa Tume Huru ya Uchaguzi Mkoa wa Simiyu, Pius Ngaiza akizungumza na Nipashe alieleza kutokupokea taarifa hizo za watu kuondolewa katika vituo vya kujiandisha na kuahidi kufuatilia katika eneo hilo na kulipatia ufumbuzi.

"Mwenyewe taarifa hizi ninazipata kutoka kwako, hivyo hapa ndiyo unanieleza na mimi ninaanza ufuatiliaji kwa watu walioko katika eneo hilo husika," alisema Ngaiza.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Fauzia Ngatumbura pamoja na Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Kenan Kihongosi walipotafutwa na mwandishi wa habari hii kwa njia ya simu, ili kutoa ufafanuzi kuhusu operesheni hiyo, simu zao ziliita pasi na kupokewa na



Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF DAR ES SALAAM
*(AT KISUTU)*

CRIMINAL CASE NO. 19336 OF 2024

THE REPUBLIC

VERSUS

CATHERNIE DOMICI LUWUMBA.....................................ACCUSED PERSON

To:
Catherine Dominic Luwumba
Plot No. 12, Block 2, Mivumoni Area,
Kinondoni Municipality
Dar Es Salaam City

WHEREAS your attendance is necessary to answer to a charge on ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM TO UNDERTAKE CONSTRUCTION WORKS CONTRARY TO SECTION 22(4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT CAP. 235 OF THE LAWS

YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE name of the Republic to appear in this Court on the 13th day of September 2024 at 08:00 am Or so soon thereafter as the case can be heard.

Here in fail not.

GIVEN under my hand and the Seal of the Court this 2nd day of August 2024

RESIDENT MAGISTRATE

This summons has been issued on the Application of the Prosecution


Served Upon Me/us:

Name.........................................

Signature.........................................

Qualification/Relationship

Date.........................................



Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF DAR ES SALAAM
*(AT KISUTU)*

CRIMINAL CASE NO. 19330 OF 2024

THE REPUBLIC

VERSUS

VITUS EBIUT NDELWA............................................ACCUSED PERSON

To:
Vitus Ebiut Ndelwa
Kituo Kipya, Gongo la Mboto Area,
Ilala Municipality
Dar Es Salaam City

WHEREAS your attendance is necessary to answer to a charge on ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM TO UNDERTAKE CONSTRUCTION WORKS CONTRARY TO SECTION 22(4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT CAP. 235 OF THE LAWS

YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE name of the Republic to appear in this Court on the 13th day of September 2024 at 08:00 am Or so soon thereafter as the case can be heard.

Here in fail not.

GIVEN under my hand and the Seal of the Court this 2nd day of August 2024

RESIDENT MAGISTRATE

This summons has been issued on the Application of the Prosecution

Served Upon Me/us:

Name.........................................

Signature.........................................

Qualification/Relationship

Date.........................................

# TAWA yawaswaga tembo 500 waliovamia makazi ya watu

**Na Joseph Mwendapole**

MAMLAKA ya Usimamizi wa Wanyamapori (TAWA) imefanikiwa kuwarejesha katika maeneo yao ya hifadhi tembo 500 waliovamia makazi ya watu na kuhatarisha maisha yao.

Hayo yalielezwa mwishoni mwa wiki na Ofisa Uhifadhi wa TAWA, Isaac Chamba, wakati wa semina ya wahariri wa vyombo vya habari iliyoandaliwa na Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira (JET) wilayani Bagamoyo, mkoani Pwani.

Kongamano hilo lilijadili mradi unaotekelezwa na serikali wa Kukabiliana na Migongano ya Binadamu na Wanyamapori unaofadhiliwa na Shirika la Maendeleo ya Ujerumani (GIZ).

Alisema kuwa mwaka 2023/24, zaidi ya tembo 500 waliondolewa katika makazi ya watu na kurejeshwa hifadhini kutoka wilaya mbalimbali zikiwamo Nachingwea, Liwale, Bunda, Same, Mvomero na Mbarari.

"Waliswagwa kwa kutumia helikopta kuwaweka katika hifadhi jirani na walikokuwa na imesaidia sana wananchi kuishi kwa amani na kuondokana na hofu iliyokuwapo kuhusu tembo hao katika maeneo yao kwani mbali na uhalibifu wa mazao pia walikuwa wanahatarisha usalama wao," alisema

Alisema hatua hiyo pia iliokoa maisha ya tembo hao ambao kama wangeachwa waendelee kuwapo katika maeneo hayo wangeuawa na wananchi wenye hasira ambao waliharibiwa mashamba yao.

Katika hatua nyingine, ofisa huyo alisema kuwa mwaka 2023/24, TAWA iliua wanyama walioonesha tabia ya kuhatarisha usalama wa wananchi, wengi wakiwa ni kiboko na mamba ambao walivamia makazi ya watu.

Alisema Sheria Na. 283 ya Uhifadhi wa Wanyamapori, kifungu cha 73, kinatoa mamlaka kwa ofisa wa wanyamapori kuua mnyamapori yeyote anapohatarisha maisha ya watu.

Alisema katika kukabiliana na uhalibifu wowote, askari wa TAWA hulazimika kuwaua na katika kipindi ha mwaka 2023/24 wanyamapori 221 waliuawa ili kulinda maisha ya wananchi.

"Sisi TAWA maisha ya binadamu tunayapa kipaumbele kuliko mnyama yeyote yule, hivyo mnyama anapohatarisha maisha ya watu tunamdhibiti na ikiwezekana kumuua ili watu waendelee kuishi kwa amani," alisema.


Mkurugenzi Mkuu wa JET, Dk. John Chikomo, alisema Mradi wa Kupunguza Migongano Baina ya Binadamu na Wanyamapori umelenga ukanda wa Ruvuma na Lindi, hasa wilaya za Tunduru, Namtumbo na Liwale.

Alisema JET imekuwa inafundisha waandishi wa habari na wahariri namna bora ya kuandika migongano baina ya binadamu na wanyamapori katika maeneo mbalimbali nchini.

Alisema mradi huo unatekelezwa na Serikali ya Tanzania kwa ufadhili wa Serikali ya Ujerumani.

Alisema JET imekuwa inaendesha midahalo mbalimbali kuelimisha umma kuhusu mradi huo na kwamba tayari imeshafanya mdahalo mmoja kwenye televisheni na imebaki midahalo mitatu.

"JET pia inapeleka waandishi wa habari katika maeneo ya migongano baina ya binadamu na wanyamapori na tumeshakwenda Tunduru na tunatarajia kwenda maeneo mengine manne na watakaokwenda ni wale waliopata mafunzo," alisema Dk. Chikomo.



Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF DAR ES SALAAM
*(AT KISUTU)*

CRIMINAL CASE NO. 19326 OF 2024

THE REPUBLIC

VERSUS

FEISAL SALUM SELEMAN............................................ACCUSED PERSON

To:
Feisal Salum Seleman
Magomeni Mapipa Area, Magomeni WARD
Kinondoni Municipality
Dar Es Salaam City

WHEREAS your attendance is necessary to answer to a charge on ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM TO UNDERTAKE CONSTRUCTION WORKS CONTRARY TO SECTION 22(4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT CAP. 235 OF THE LAWS

YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE name of the Republic to appear in this Court on the............ day of.............................. 2024 at 08:00 am Or so soon thereafter as the case can be heard.

Here in fail not.

GIVEN under my hand and the Seal of the Court this ........................ day of ............................. 2024

RESIDENT MAGISTRATE

This summons has been issued on the Application of the Prosecution

Served Upon Me/us:

Name.........................................

Signature.........................................

Qualification/Relationship

Date.........................................

HABARI KITAIFA

# Ulega aanika faida mkutano wa OACPS

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, amesema kufanyika kwa mkutano wa OACPS nchini Tanzania kutasaidia kuweka mikakati madhubuti ya kuinua sekta ya uvuvi na kuchechemua uchumi wa taifa kwa ujumla.

Alisema hayo wakati akifungua Mkutano wa Wataalam wa Uvuvi wa Bahari na Maji baridi kutoka nchi wanachama wa Umoja wa Afrika, Karibiani na Pasifiki (OACPS), jijini Dar es Salaam, jana.

"Lengo la mkutano wa OACPS ni kujadili mambo mbalimbali yanayohusu ustawi wa bahari na maji baridi na kuweka mikakati ya kunusuru hatma ya uvuvi na wavuvi wenyewe," alisema.

Alisema Mkutano wa OACPS utakuwa na faida nyingi nchini ikiwamo mashirika yaliyoshiriki kuangalia namna ya kuwawezesha wavuvi wadogo kuboresha shughuli zao kwa kuzingatia mabadiliko ya tabia nchi.

Kuwawezesha wavuvi kutumia teknolojia za kisasa za uvuvi ili kuwaondoa kutoka katika uvuvi wa kienyeji na wapate vifaa vya kisasa vya uvuvi.

Kadhalika alisema mkutano huo utatoa fursa kwa wadau wa uvuvi kubadilishana uzoefu ili kwa pamoja waweze kuboresha shughuli zao.

"Serikali ya Tanzania inayoongozwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imefanya jitihada kubwa katika kujaribu kutatua changamoto zinazowakumba wavuvi wadogo na wakuzaji viumbe maji ikiwa ni pamoja na kuboresha miundombinu ya uvuvi, kuboresha teknolojia, kutoa vifaa vya kisasa kwa ajili ya shughuli za uvuvi na ukuzaji viumbe maji na kuweka mazingira mazuri kwa ajili ya kupata mitaji na masoko," alisema.

Aidha, Waziri Ulega alibainisha kuwa Tanzania itaendelea kusimamia ipasavyo juhudi zitakazohakikisha usimamizi endelevu wa rasilimali za bahari na maji ya ndani zinazofanyika kupitia mikakati mbalimbali iliyoandaliwa ikiwamo kupitia Mpango Kabambe wa Sekta ya Uvuvi, Sera ya Uchumi wa Buluu, na juhudi zetu zinazoendelea za kupambana na uvuvi Haramu na usioripotiwa (IUU), ambayo inalenga kuhakikisha kuwa rasilimali za maji hasa bahari, maziwa na mito zinaendelea kuwa endelevu na kunufaisha kizazi cha sasa na kijacho.



Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega akifungua mkutano wa OACPS. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ugomvi mume, mke wasababisha kifo cha kichanga wa miezi saba

**Na Steven William,** MUHEZA

JESHI la Polisi mkoani Tanga linamsaka Dismas Yohana, mkazi wa Kijiji cha Kwafungo, wilayani Muheza kwa tuhuma za kusababisha kifo cha mtoto wake, Aloni Dismas mwenye umri wa miezi saba.

Kamanda wa Polisi mkoani Tanga, Almachius Mchunguzi alisema jana kuwa Yohana anadaiwa kusababisha kifo cha mtoto wake wakati anagombana na mkewe, Sharifa Omari, ndipo alimwangukia mtoto huyo aliyekuwa amelala kitandani.

Kamanda Muchunguzi alisema tukio hilo lilitokea juzi usiku katika kijiji hicho ambako mtuhumiwa huyo alikuwa anaishi na familia yake.

Alisema Jeshi la Polisi linaendelea na uchunguzi wa tukio hilo kubaini chanzo cha ugomvi.

Mmoja wa ndugu wa familia, Matha Joseph alisema kuwa ulitokea ugomvi usiku kati ya wanandoa hao uliosababisha kupigana na kumwangukia mtoto wao huyo ambaye alikimbizwa Hospitali Teule ya Muheza, lakini alifariki dunia.

Alisema kuwa baada ya ugomvi wa wanandoa hao, mke aliondoka nyumbani usiku majira ya saa mbili mpaka Kituo cha Polisi Muheza Mjini kutoa taarifa, kisha kwenda Hospitali Teule ya Muheza kwa ajili ya matibabu ya mtoto.

Alisema kuwa ilipofika saa tano usiku, mtoto huyo alifariki dunia na mama yake alitibiwa na kupewa rukhsa kwenda nyumbani.

Alisema kuwa mtoto huyo ameshazikwa katika Kijiji cha Maskati, Kata ya Bwembwera, wilayani Muheza na kwamba mtuhumiwa ametoroka, anatafutwa na Jeshi la Polisi.


SIMBA CEMENT
Heidelberg Materials

## UNAUDITED RESULTS FOR THE QUARTER ENDED 30 JUNE 2024
## CHAIRMAN'S STATEMENT

**Dear Shareholders,**

We present the unaudited quarterly results of Tanga Cement Public Limited Company and its subsidiary for the quarter ended 30th June 2024. In overall, during the first half of the year, the industry was impacted by adverse weather condition as well as the delays from government funded infrastructure projects.

During this period, April – June 2024, Company's revenue declined by 10% compared to the same period in 2023. Operational costs declined by 24% and operating profit increased by 53% compared to April – June 2023. This achievement is attributed to several initiatives taken by the management to improve operational efficiencies and costs reduction.

Loss before tax increased from TZS 2.576 million to TZS 9.923 million mainly due to the impact from the interest expense on borrowing and foreign exchange losses due to the translation of the facility dominated in foreign currency.

Net cash flows from financing activities increased significantly due to additional short-term working capital needs, which were necessary to meet increased working capital requirements. This increase in working capital requirements coupled with decline in revenue led to a net cash outflow from operating activities.

The management is optimistic on the positive market outlook in the second half of the year. Market conditions are expected to improve and infrastructure projects to pick-up during the second half of the year.

**Appreciation**
Tanga Cement is grateful to its staff and customers as it strives to achieve its growth strategy. With Tanzania's significant role in the East African construction market, cement output is expected to increase, positioning Tanga Cement to capitalize on regional market growth opportunities. We affirm our commitment to stakeholders through our high-quality cement and clinker and our contribution to Tanzania's sustainable growth.

For and on behalf of the Board.

Hakan Gurdal — Chairman of the Board
Christian Mikli — Board Member
Quresh Ganijee — Company Secretary

CONSOLIDATED AND SEPARATE STATEMENTS OF PROFIT OR LOSS AND OTHER COMPREHENSIVE INCOME
FOR THE PERIOD ENDED 30 JUNE 2024

| | Group Jun-24 TZS '000' | Group Jun-23 TZS '000' | Company Jun-24 TZS '000' | Company Jun-23 TZS '000' |
|---|---|---|---|---|
| Revenue from contracts with customers | 49,358,948 | 55,030,505 | 49,358,948 | 55,030,505 |
| Cost of sales | (31,442,314) | (40,950,893) | (31,456,479) | (40,950,892) |
| **Gross profit** | **17,916,634** | **14,079,612** | **17,902,469** | **14,079,613** |
| Other income | 36,753 | 49,965 | 32,698 | 47,863 |
| Other expenses | (138,517) | - | (138,517) | - |
| Selling expenses | (525,217) | (843,964) | (525,217) | (843,964) |
| Administration expenses | (5,948,553) | (4,214,232) | (5,920,285) | (4,389,324) |
| Depreciation charge | (4,974,138) | (4,852,768) | (4,961,654) | (4,870,088) |
| Impairment and other charges | - | 10,224 | - | 10,224 |
| Decrease/ (increase) in expected credit losses | (243,661) | 224,779 | (243,661) | (26,101) |
| **Operating profit** | **6,123,301** | **4,453,616** | **6,145,833** | **4,008,223** |
| Interest expense | (9,002,080) | (6,341,771) | (9,002,080) | (6,344,028) |
| Finance income | - | 10,774 | - | 10,774 |
| Foreign exchange and fair value losses | (7,066,197) | (242,244) | (7,067,267) | (251,409) |
| **Loss before tax** | **(9,944,976)** | **(2,119,625)** | **(9,923,514)** | **(2,576,440)** |
| Income tax (charge)/credit | (293,888) | (294,820) | (293,888) | (294,820) |
| **Loss for the period** | **(10,238,864)** | **(2,414,445)** | **(10,217,402)** | **(2,871,260)** |

TANGA CEMENT PUBLIC LIMITED COMPANY

CONSOLIDATED AND SEPARATE STATEMENTS OF FINANCIAL POSITION
AS AT 30 JUNE 2024

| | Group Jun-24 TZS '000' | Group Jun-23 TZS '000' | Company Jun-24 TZS '000' | Company Jun-23 TZS '000' |
|---|---|---|---|---|
| **ASSETS** | | | | |
| **Non-current assets** | | | | |
| Property, plant and equipment | 268,460,078 | 281,560,529 | 268,457,846 | 280,828,827 |
| Right-of-use assets | 248,844 | 4,618,068 | 248,844 | 4,616,876 |
| Investment property | 987,848 | 503,664 | - | - |
| Investment in subsidiary | - | - | 420,995 | 420,995 |
| Financial asset - Interest rate cap | - | 7,864,730 | - | 7,864,730 |
| | **269,696,770** | **294,546,991** | **269,127,685** | **293,731,428** |
| **Current assets** | | | | |
| Due from employees' share trust | - | - | 1,490,682 | 773,467 |
| Inventories | 68,616,138 | 87,781,303 | 68,616,138 | 87,781,303 |
| Trade and other receivables | 11,033,017 | 4,973,101 | 11,044,615 | 5,151,031 |
| Current income tax recoverable | 10,588,817 | 8,689,931 | 10,052,631 | 8,186,454 |
| Cash and bank balances | 16,706,521 | 8,532,201 | 16,571,158 | 8,453,994 |
| | **106,944,493** | **109,976,536** | **107,775,224** | **110,346,249** |
| **TOTAL ASSETS** | **376,641,263** | **404,523,527** | **376,902,909** | **404,077,677** |
| **EQUITY AND LIABILITIES** | | | | |
| **Equity** | | | | |
| Issued capital | 1,273,421 | 1,273,421 | 1,273,421 | 1,273,421 |
| Treasury shares | (1,490,682) | (773,466) | - | - |
| Retained earnings | (1,334,578) | 105,739,874 | (2,274,827) | 104,046,042 |
| **Equity attributable to owners of the parent** | **(1,551,839)** | **106,239,829** | **(1,001,406)** | **105,319,463** |
| **Total equity** | **(1,551,839)** | **106,239,829** | **(1,001,406)** | **105,319,463** |
| **Non-current liabilities** | | | | |
| Lease liabilities | 273,907 | 4,508,395 | 273,907 | 4,412,199 |
| Provision for site restoration | 30,325 | 30,014 | 30,325 | 30,014 |
| Term borrowings: Non-current portion | 258,018,093 | 221,398,551 | 258,018,093 | 221,398,551 |
| Deferred tax liability | 950,783 | 950,784 | 950,783 | 950,784 |
| | **259,273,108** | **226,887,744** | **259,273,108** | **226,791,548** |
| **Current liabilities** | | | | |
| Lease liabilities | 36,393 | 673,668 | 36,393 | 659,294 |
| Trade and other payables | 46,242,512 | 43,084,354 | 45,953,725 | 43,308,995 |
| Contract liabilities | 8,387,524 | 8,636,370 | 8,387,524 | 8,996,815 |
| Short-term borrowings | 45,512,096 | - | 45,512,096 | - |
| Bank overdrafts | 18,741,469 | 19,001,562 | 18,741,469 | 19,001,562 |
| | **118,919,994** | **71,395,954** | **118,631,207** | **71,966,666** |
| **Total liabilities** | **378,193,102** | **298,283,698** | **377,904,315** | **298,758,214** |
| **TOTAL EQUITY AND LIABILITIES** | **376,641,263** | **404,523,527** | **376,902,909** | **404,077,677** |

TANGA CEMENT PUBLIC LIMITED COMPANY

CONSOLIDATED AND SEPARATE STATEMENTS OF CASH FLOWS
FOR THE PERIOD ENDED 30 JUNE 2024

| | Group Jun-24 TZS '000' | Group Jun-23 TZS '000' | Company Jun-24 TZS '000' | Company Jun-23 TZS '000' |
|---|---|---|---|---|
| **OPERATING ACTIVITIES** | | | | |
| Cash generated from operating activities | (2,611,697) | 8,966,256 | (2,678,204) | 9,173,553 |
| Interest income received | - | 842,447 | - | 842,447 |
| Income taxes paid | (2,037,999) | (805,679) | (2,037,999) | (788,637) |
| **Net cash flows (used)/from operating activities** | **(4,649,696)** | **9,003,024** | **(4,716,203)** | **9,227,363** |
| **INVESTING ACTIVITIES** | | | | |
| Purchase of property, plant and equipment | (4,452,006) | (3,356,755) | (4,452,006) | (3,356,755) |
| **Net cash flows used in investing activities** | **(4,452,006)** | **(3,356,755)** | **(4,452,006)** | **(3,356,755)** |
| **FINANCING ACTIVITIES** | | | | |
| Principal repayments - lease liabilities | (176,632) | (155,536) | (176,632) | (155,536) |
| Interest paid - overdrafts | (1,615,785) | (949,050) | (1,615,785) | (949,050) |
| Interest paid - term borrowings | (416,024) | - | (416,024) | - |
| Short-Term Loan proceeds | 43,672,061 | - | 43,672,061 | - |
| **Net cash flows from/(used) in financing activities** | **41,463,620** | **(1,104,586)** | **41,463,620** | **(1,104,586)** |
| **Net increase in cash and cash equivalents** | **32,361,918** | **4,541,683** | **32,295,411** | **4,766,022** |
| Net foreign exchange differences | - | (483,249) | - | (727,476) |
| Cash and cash equivalents at 1 January | (34,396,866) | (14,527,795) | (34,465,722) | (14,586,114) |
| **Cash and cash equivalents at end of period** | **(2,034,948)** | **(10,469,361)** | **(2,170,311)** | **(10,547,568)** |

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Matukio ya utekaji, mauaji yanafikirisha

**KURIPOTIWA** kwa matukio ya utekaji na mauaji ya kila mara katika maeneo mbalimbali nchini yanaleta hali ya wasiwasi na amani iliyozoeleka imeanza kuingia doa.

Tanzania inasifika duniani kuwa ni nchi ya amani na ndio sababu wageni wengi wanamiminika kuja kuitembelea.

Matukio haya yaliyoanza kujitokeza yanaleta hali ya wasiwasi na kusababisha wananchi kukosa amani wanapofanya shughuli zao kwa kuwa hawajui ni wakati gani wanaweza kupatwa na mkasa.

Tanzania haikuzoea kusikia kila kukicha matukio ya kutisha na ya kusikitisha yakiwamo ya utekaji, ubakaji na mauaji.

Kuibuka kwa matukio haya kumesababisha kila mtu kumnyooshea kidole mwenzake bila kujua kiini cha tatizo hilo ni nini.

Takribani miaka mitatu iliyopita kuliibuka matukio ya watu kutoweka wakiwamo waandishi wa habari na wengine mpaka leo hawajulikani walipo.

Hali ilirudi kuwa shwari, lakini sasa yameanza kuibuka tena na kwenye jamii yamepamba moto kutokana na taarifa zinazoripotiwa kila mara matukio hayo kufanyika.

Kinachosikitisha zaidi hata watoto wasiokuwa na hatia wameingizwa kwenye matukio hayo na kupotezewa maisha yao.

Taarifa za hivi karibuni zinaeleza mtoto na mama yake walivyofanyiwa vitendo vya ukatili na kisha kuuawa.

Kwa hivi karibuni Mkoa wa Dodoma, kumeripotiwa matukio kadhaa ya kinyama na mauaji na watu kuhoji kuna upepo gani mbaya umeikumba nchi yetu.

Wanaotekeleza unyama huo haifahamiki kama wanafanya kwa kulipiza kisasi au kwa sababu za kishirikina.

Wakati uchunguzi ukiendelea kwa matukio yaliyofanyika katika mkoa huo, mengine yanajitokeza ya utekaji wa kada wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), ambaye ilidaiwa alichukuliwa na watu wasiojulikana wakati akiwa kwenye basi la abiria.

Huku Jeshi la Polisi likifanya uchunguzi kuhusu tukio hilo, habari zinaeleza kuwa kada huyo amekutwa ameuawa eneo la Ununio, jijini Dar es Salaam.

Hakika tukio hili limezua taharuki kubwa kwa kuwa inaelezwa kuwa, waliomchukua walikuwa wamebeba silaha za moto na walimfunga pingu kabla ya kumshusha kwenye basi hilo alilokuwa akisafiri nalo.

Watu kutekwa, kutoweka na kuondolewa uhai sasa zimekuwa taarifa zinazotawala vyombo vya habari pamoja na mitandao ya kijamii.

Matukio haya yalianza taratibu, lakini yanakoendelea yanaweza kuwa makubwa na kusababisha wananchi kuhofia kutembea kwa amani kwenye nchi yao.

Jeshi la Polisi linafanya uchunguzi kuhusu matukio hayo na imani ya wananchi kuwa waliofanya vitendo hivyo vya kinyama watakamatwa ili sheria ichukue mkondo wake.

Damu za watu haziwezi kupotea bure, hata kama waliofanya vitendo hivyo watakuwa wamekimbia kwenda maeneo ya mbali, lazima watajulikana.


Wananchi pia ni lazima tutoe ushirikiano kulisaidia Jeshi la Polisi kuwapata wahalifu hao ili nchi yetu isiingie doa.

Sisi sote ni walinzi na tunapotoa ushirikiano kazi ya kupatikana kwa wahalifu hao itakuwa rahisi. Hakuna anayependa kuona uhai wa mtu ukiondolewa kwa sababu za chuki na ubinafsi au ushirikina.

Tanzania ni nchi ya kisiwa cha amani na amani hii iendelee kudumishwa ili tuendelee kupokea wageni wanaokuja kujifunza kwetu jinsi ya kuishi kwa umoja na upendo.

**Mungu ibariki Tanzania, Mungu ibariki Afrika.**

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Kiswahili ni muhimu kwenye TEHAMA

Na Sabato Kasika

**MATUMIZI** ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), yaliyoenea dunia nzima, ni hatua muhimu ya kuenea lugha mbalimbali zikiwamo za kimataifa na kikanda.

Kwa sasa, lugha nyingine za Kiafrika mfano Kiswahili kinachozungumzwa karibu ukanda wote wa Afrika Mashariki , Kusini na Kati, Kichewa kinachotumika na raia wengi wa Zambia, Zimbabwe na Malawi ni miongoni mwa zile zinazosambaa kwa kasi.

Kiswahili kimeenea kikitumiwa na walimu katika kufundisha na kujifunza kwenye baadhi ya shule na vyuo vikuu sehemu nyingi duniani, mfano Afrika Mashariki, China na Marekani.

Lugha hii ya taifa, imekuwa na umuhimu katika ufundishaji na ujifunzaji wa TEHAMA, kwa sababu inawarahisishia walimu na wanafunzi kuielewa vizuri teknolojia hiyo kwa lugha waliyoizoea.

Hivyo, ninaamini kuna umuhimu mkubwa wa kuendelea kutumia lugha hiyo, katika TEHAMA, kwani ni njia inayoweza kumfanya mwanafunzi afurahie somo kwa kujifunza kwa lugha anayoielewa kwa ufasaha.

Ikumbukwe kuwa lengo la kuanzisha somo la TEHAMA ni kumwezesha mwanafunzi kuimarisha mbinu zake za kupata habari na mawasiliano yaliyoboreshwa katika kujielimisha na kujiendeleza kiuchumi, kisiasa na kijamii kwa kutumia teknolojia ya asili na ya kisasa.

Hivyo, uamuzi wa kutumia Kiswahili kufundishia, ninaamini unaweza kuleta manufaa makubwa, sio tu katika kuendeleza Kiswahili kama lugha ya taaluma, bali pia kuboresha TEHAMA.

Serikali imekuwa ikigawa vifaa vya TEHAMA, vikiwamo vishikwambi, kwa walimu wote na kuwapa mafunzo ya jinsi ya kuvitumia ili kuboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji.

Ninaamini kwamba, katika ulimwengu wa sasa wa maendeleo ya Sayansi na Teknolojia, matumizi ya TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji ni nyenzo muhimu itakayorahisisha utoaji elimu bora.

Vilevile, matumizi ya Kiswahili kufundishia stadi za msingi za TEHAMA, ni hatua ya mwanzo kuelekea kwenye matumizi ya lugha ya Kiswahili kutolea mafunzo ya kiufundi.

Somo la TEHAMA lilianzishwa katika mtaala mpya wa Elimu ya Msingi (Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, 2005), ili kumpa mwanafunzi maarifa na stadi za matumizi ya habari, vyombo vya mawasiliano.

Hivyo, kutumia Kiswahili kama lugha ya kufundishia somo la TEHAMA ni kukifanya kuwa nyenzo ya kuwasilishia elimu ya sayansi na teknolojia ya kisasa, kwani lengo ni kuwasilisha stadi, mielekeo ya maarifa ambayo yamekusudiwa kwa kutumia lugha hiyo ya taifa.

Jambo la muhimu, ni serikali kuendelea kuandaa mafunzo ya kuwajengea walimu uelewa zaidi wa matumizi sahihi ya vifaa hivyo vya TEHAMA ili nao wawafundishe wanafunzi kwa ajili ya kuandaa wataalam wengi wa baadaye wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano.

Lakini pamoja na hayo, kumekuwapo na taarifa kwamba vifaa vingi vya TEHAMA katika baadhi ya shule za msingi zilizowahi kuboreshwa na kuwekwa vifaa hivyo, haviko katika hali nzuri.

Inaelezwa kuwa hali hiyo inatokana na utunzaji wa vifaa hivyo kutokuwa mzuri lakini pia watumiaji wake kutokuwa makini na hivyo kusababisha viharibike mapema vingali vipya.

Ninadhani ingekuwa ni vyema, wakati Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ikiendelea na mchakato wa kununua vifaa vya TEHAMA kwa ajili ya vituo vya walimu na vingine maalumu vitakavyochaguliwa kutumiwa na walimu kwenye ufundishaji na ujifunzaji ili kurahisisha utoaji elimu bora na yenye ufanisi nchini, vilivyopo vingetunzwa vizuri.

Kwa kuwa serikali inazidi kuboresha sekta ya elimu ikiwamo kujenga na kukarabati miundombinu kuanzia madarasa, nyumba za walimu na ofisi za walimu, kutoa mafunzo kazini kwa walimu na kununua vifaa vya kufundishia na kujifunzia, ninadhani tatizo hilo pia litashughulikiwa.

TANGAZO


TRA

TANZANIA REVENUE AUTHORITY

# WASILIANA NA KAMISHNA MKUU WA TRA KUPITIA SIKIKA APP

## Namna ya Kutumia

1. Ingia katika simu janja yako ya Android au IOS (Apple iphone au Ipad), kisha nenda sehemu ya kupakulia programu (Google play store au App Store) kisha tafuta programu ya 'TRA SIKIKA'.

2. Pakua 'TRA SIKIKA' kutoka Google Playstore kwa watumiaji wa simu za ANDROID, na kwa watumiaji wa simu za IOS (Apple Iphone au Ipad) pakua kutoka APP STORE.

3. Fungua 'SIKIKA APP' ambapo kurasa mbili za kwanza ni za kukukaribisha pamoja na ujumbe mfupi kutoka 'SIKIKA APP' (Welcome Message / App Intro).

4. 'SIKIKA APP' inakuwezesha kutuma maoni au malalamiko pamoja na kuyafuatilia.

5. Kutuma maoni bonyeza kitufe cha maoni , kisha andika maoni yako na bonyeza kitufe cha wasilisha. Utapata ujumbe wa maoni yako kupokelewa pamoja na Namba ya Kufuatilia (Track Number).

6. Kutuma malalamiko bonyeza kitufe cha malalamiko , kisha andika malalamiko yako na bonyeza kitufe cha wasilisha. Utapata ujumbe wa kupokelewa kwa malalamiko yako pamoja na namba ya kufuatilia (Track Number).

7. Kufuatilia maoni au malalamiko bonyeza kitufe cha fuatilia kisha ingiza namba uliyopewa baada ya kutuma maoni au malalamiko kisha bonyeza kitufe cha tuma. (Utapokea Ujumbe kuhusu utekelezaji wa Maoni au Malamiko yako).

TRA

## TRA SIKIKA APP






Mwakilishi kutoka Taasisi ya International Finance Corporation (IFC), Anna Mushi (wa pili kushoto) akimkabidhi tuzo Meneja Uhusiano na Mawasiliano kutoka GGML, Stephen Mhando (wa kwanza kushoto) kwa kutambua mchango wa kampuni hiyo katika kuunga mkono jitihada za kufikia malengo ya maendeleo endelevu (SDG). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mawaziri kikaangoni kero ya maji, afya

**Na Salome Kitomari,**
SIMANJIRO

MAWAZIRI wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa na Waziri wa Maji, Juma Aweso, jana walilazimika kutoa ahadi ya utatuzi wa kero ya muda mrefu ya ukosefu wa maji na huduma za afya ndani ya eneo la uchimbaji madini la Mirerani.

Kero hizo ziliibuliwa na Mbunge wa Jimbo la Simanjiro, Christopher Ole Sendeka, wakati wa mkutano wa hadhara wa Katibu wa NEC, Itikadi, Uenezi na Mafunzo ya CCM ambaye yupo kwenye ziara kukagua utekelezaji wa ilani ya chama, kusikiliza kero za wananchi, kuangalia uhai wa chama na kuhamasisha wananchi kushiriki uchaguzi wa serikali za mitaa.

Makalla alimpigia simu Waziri Mchengerwa na kumwambia wanaomba kujengewa zahanati yenye hadhi ya kituo cha afya ili wachimbaji na wafanyakazi wengine kupata huduma za afya.

"Tunategemea kutoka kwako namna ya kuwasaidia hawa wananchi wenye mapenzi mema na Rais Samia Suluhu Hassan," alisema.

Mchengerwa alisema dhamira ya Rais Samia ni kuona Watanzania wanapata huduma za afya kwa karibu na kwamba yeye kama msimamizi wa afya ya msingi atawaelekeza wataalam kwenda kufanya tathmini na Katibu Mkuu kutenga fedha Sh. milioni 200 kwa ajili kuanza ujenzi wa majengo.

Aidha, Mchengerwa aliahidi kutembelea eneo hilo na kwamba kwa mwaka huu wa fedha itatengwa ili wananchi wapate huduma kwenye makazi yao au wanapofanyia kazi na lazima watekeleze kwa kuwa ni utekelezaji wa Ilani ya CCM.

Kuhusu tatizo la maji, Makalla alisema alizungumza na Waziri wa Maji, Aweso ambaye alisema utatuzi wa muda mfupi kutatua shida ya maji ndani ya eneo la Mirerani wameweka bomba la maji na kutakuwa na magari yatakayochota na kulepeka kwa wananchi.

"Wito wetu wananchi waweke vifaa vya kuhifadhia maji, yatabeba kwenye kituo yanakuletea. Huu ni utaratibu wa muda mfupi hadi maji yatakaposambazwa ndani ya ukuta wa Mirerani," alisema mwakilishi wa RUWASA.

> **"Wito wetu waweke vifaa vya kuhifadhia maji, yatabeba kwenye kituo yanakuletea. Huu ni utaratibu wa muda mfupi hadi maji yatakaposambazwa ndani ya ukuta wa Mirerani," alisema mwakilishi wa RUWASA.**

Kuhusu barabara za ndani ya eneo la mgodi, Makalla alisema aliongea na mtendaji wa Wakala wa Barabara za Vijijini (TARURA) ambaye ameahidi akirudi kutoka safari atatembelea eneo hilo ili wajipange namna ya kutatua.

Alisema Ilani ya Uchaguzi 2020-2025 imetekelezwa vizuri na hakuna awamu kama ya Rais Samia Suluhu Hassan ambaye amepeleka fedha nyingi za kutekeleza miradi ya maendeleo.

"CCM ina wajibu wa kusikiliza na kutatua kero za wananchi, hata kama tunakwenda kwenye Uchaguzi wa Serikali za Mitaa Nawaaminisha changamoto zilizopo zitatatuliwa na CCM," alisema.

Makalla ambaye amewahi kuwa Mkuu wa Mkoa wa Manyara, alisema katika ziara kwenye mikoa 17 wamebaini kwamba CCM ni imara kuliko wakati wowote, na kinaendelea kuaminiwa kutokana na sera na utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi.

"Haihijitaji kutumia akili nyingi kuonesha vyama vingine vimepoteza mwelekeo ndio maana kila kukicha wanahamia CCM, hapa nimepokea wanachama 50 wenye kadi za kisasa," alisema.

Aidha, alisema uimara wa CCM unatajwa duniani kwa kuwa ndio chama kikubwa na imara namba tisa duniani,na kwa Afrika ni namba moja,huku Jarida la hivi karibuni limemtaja Rais Samia Suluhu Hassan kama kiongozi bora.

Makalla alisema kwa mfumo wa uchaguzi Tanzania ili ushike dola ni kushinda Uchaguzi wa Serikali za Mitaa ambao utafanyika Novemba 27, 2024 na Uchaguzi Mkuu Oktoba, 2025.

Awali, Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, Fakii Lulandala, alisema utekelezaji wa Ilani ya CCM ndio unawafanya wananchi wazidi kumkubali Rais Samia.

"Wakati anaingia madarakani 2021 kulikuwa na vijiji 21 tu vyenye umeme, leo vijiji 56 vimefikishiwa huduma ya umeme, maana yake kwa kipindi cha miaka 60 wamepeleka vichache ila kwa miaka mitatu wamevifikia vyote.

"Tumepokea fedha za kupeleka umeme kwenye vitongoji 27, mazingira ya Simanjiro ni tofauti na maeneo mengi kijiji hadi kingine ni kilomita 70, 50 na jirani ni 30, na kwamba tangu kuanza kwa miradi hiyo Sh. bilioni 11.7 zimetumika kupeleka umeme," alisema.

"TARURA wanapewa hadi kutoka Sh. milioni 10 hadi bilioni 4.8, kwenye maji wakati anaingia bajeti ya RUWASA ilikuwa Sh. bilioni 1.3 na sasa ni Sh. bilioni 4.2 na kuna mradi wa maji wa mji wa Mirerani wa Shilingi bilioni nne unaoendelea.

Lulandala alisema kwenye afya wilaya ilikuwa na vituo vya afya vitatu, lakini ndani ya miaka minne vimeongezeka vitano, na bajeti ijayo kuna vituo viwili vitakamilika kabla ya uchaguzi.

"Wakati tunatembelea maeneo mengi wananchi walikuwa na hofu kwa kuwa hawaletewi maendeleo basi serikali ina mpango wa kulifanya eneo hilo hifadhi, lakini aliwaambia umeme hauwezi kupelekewa tembo au fisi bali wamepelekewa watu," alisema.

Awali, Mbunge wa Jimbo la Simanjiro, Christopher Ole Sendeka, alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan, kwa fedha za miradi ya elimu, Kituo cha Afya Mirerani na mingine.

Alisema serikali imetenga fedha za ujenzi wa Shule ya Sekondari Ngiamtu na Shule ya Msingi Kata ya Mirerani ambazo zitajengwa na kukamilika kisha kukabidhiwa kwa wananchi.

Alisema vijiji 56 vya Wilaya ya Simanjiro vimefikiwa na umeme na wanaomba usambazwe hadi kwenye vitongoji.

Aliomba serikali kuangalia uwezekano wa kujenga zahanati ndani ya eneo la ukuta wa Mirerani, kupeleka huduma ya maji na ujenzi wa barabara za ndani zipite kwa mabasi na magari madogo ili kupunguza gharama kwa watumiaji.

## Wanafunzi 200 wasomea darasa moja

**Na Julieth Mkireri,**
KIBAHA

SHULE ya Msingi Lumumba yenye wanafunzi 1,407 inakabiliwa na upungufu wa vyumba vya madarasa na kusababisha mrundikano wa wanafunzi katika darasa moja.

Mwalimu Mkuu wa shule hiyo iliyoko Kata ya Pangani, Halmashauri ya Mji wa Kibaha, Juma Aeshi, alitoa taarifa hiyo wakati wa mahafali ya darasa la saba.

Aliwaambia waandishi wa habari kuwa vyumba vilivyopo kwa sasa ni vinane pekee ambavyo havikidhi mahitaji.

Aeshi alisema amefikisha ombi la kuongezewa vyumba vya madarasa na mwaka huu alipata kimoja.

Aidha, alisema kuna darasa ambalo wanafunzi wamefikia idadi ya 200 jambo lililowalazimu kutoa madawati yote ili watoshe kukaa wote na kuendelea na vipindi.

Pia, aliiomba Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) kuwaunganishia huduma ya maji ya bomba ili waachane na maji ya kisima ambayo wanayapata kwa mmoja wa wananchi na kulipia kila mwezi.

Alisema kwasasa wanadaiwa Sh. 800,000 kwa kushindwa kulipia bili kwa wakati huku michango ya wazazi kulipia deni hilo ikisuasua.

Mwenyekiti wa Kamati ya shule hiyo, Filberha Richard, alisema madarasa katika shule hiyo yanaendelea kujengwa kwa awamu, lakini bado hayajakidhi mahitaji. Pia, aliomba serikali kuangalia uwezekano wa kujenga ofisi ya walimu kwa kuwa kwasasa ipo moja ambayo haitoshi na kufanya baadhi ya walimu kufanyia kazi zao nje ya vyumba vya madarasa.

Mdau wa Maendeleo David Msuya ambaye alishiriki katika mahafali hayo aliahidi kutoa mashine ya kuchapishia mitihani ya wanafunzi yenye thamani ya Sh. 800,000.

Akizungumzia uhaba wa vyumba vya madarasa katika shule hiyo, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Kibaha, Rogers Shemwelekwa, alisema utatuzi wake umeanza kwa ujenzi wa shule nyingine karibu na iliyopo sasa.



# EU watoa masharti ununuzi kahawa ya Tanzania

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

SOKO la nchi za Jumuiya ya Umoja wa Ulaya (EU), limekuja na sheria mpya inayotaka mazao kama kahawa yanayokwenda nchi za jumuiya hiyo, yasitokane na uharibifu wa mazingira.

Kutokana na masharti hayo, Tanzania kupitia Bodi ya Kahawa (TCB), imetangaza kuanza upya kusajili wakulima wote wa kahawa katika mikoa 17 inayozalisha zao hilo.

Uamuzi wa kusajili wakulima hao ili kuendelea kutumia soko hilo la EU ambalo huchukua asilimia 50 ya kahawa yote ya Tanzania, ulitangazwa mwishoni mwa wiki na Mkurugenzi Mkuu wa TCB, Primus Kimaryo."Bodi ya Kahawa Tanzania katika kuendeleza masoko yetu ya Umoja wa Ulaya, tunaanza rasmi kusajili upya wakulima wote wa kahawa nchini. Kama mnavyofahamu soko la jumuiya hiyo, limekuja na sheria mpya inayotaka mazao, mfano kahawa yanayokwenda nchi za Ulaya yasitokane na uharibifu wa mazingira," alisema na kuongeza:

"Mazao mengine pamoja na kahawa, ni soya beens, mbao, mpira, michikichi na kakao. Katika usajili huu ambao tutaufanya, tunategemea kwamba kila mkulima anayelima kahawa atasajiliwa kwa kuonesha kitambulisho chake, kupigwa picha yake,".

**"Naomba wakulima kutumia fursa hii kama mojawapo ya mkakati mahususi wa kuendelea kutumia soko letu la EU. Usajili huu tunategemea kuanza Septemba mwaka huu katika Mkoa wa Kagera..."**

Alisema vilevile mkulima atachukuliwa alama za shambani mwake; na namna gani analima kahawa yake na amelima kahawa hiyo kutokea mwaka gani.

Alisema taarifa hizo ni muhimu kwa kuwa zinatoa vielelezo kwamba kahawa inayozalishwa Tanzania haitokani na uharibifu wa mazingira.

Alisema katika kutekeleza jambo hilo aliomba ushirikiano na halmashauri za wilaya katika halmashauri zote zinazolima kahawa nchini.

Kimaryo alisema zoezi hilo ni la haraka kwa kuwa kuanzia Januari Mosi mwakani mazao hayo yanayokwenda EU yanatakiwa yathibitishwe kwamba hayajatokana na uharibifu wa mazingira.

Aidha, alisema serikali kupitia Wizara ya Kilimo, itaendelea kuwasiliana kwa namna inavyoona inafaa na EU kuhusiana na mambo mengine, kwa mfano matumizi ya viuatilifu, upatikanaji wa mbegu na ufanyaji wa kazi katika mashamba mbalimbali nchini. "Naomba wakulima kutumia fursa hii kama mojawapo ya mkakati mahususi wa kuendelea kutumia soko letu la EU. Usajili huu tunategemea kuanza Septemba mwaka huu katika Mkoa wa Kagera ambapo zaidi ya asilimia 40 ya kahawa yetu inatoka Mkoa huo, tutakwenda Mkoa wa Songwe na Ruvuma," alisema na kuongeza:

"Halafu tutakuja Mkoa wa Kilimanjaro, Manyara na Arusha. Mikoa mingine itafuata baadae kulingana na jinsi hali ya masoko inavyoendelea. Serikali imejipanga kutumia mifumo yake ya usajili kwa kushirikisha wadau, ambapo katika kila halmashauri tutawatumia maofisa ushirika, maofisa kilimo walioko kwenye kila halmashauri katika kusaidia katika kusaidia ufanikishaji wa zoezi hili," alisema.

Alisema TCB itashirikisha pia wanafunzi wa vyuo vikuu, ambao wanajua utumiaji wa vifaa maalum vya mipaka ya mashamba, aidha maofisa ugani walioko maeneo hayo na maofisa tarafa.

Kaya 400,000 Tanzania zinalima kahawa, huku asilimia 90 ya wazalishaji wakiwa ni wakulima wadogo. Pia Tanzania inategemea uzalishaji wa zao hilo katika hekta 220 zilizoko mikoa 17.




Ofisa Elimu Shule za Awali na Msingi wilaya ya Muheza mkoani Tanga, Pili Maxmiliani akitoa taarifa ya maandalizi ya mtihani wa taifa wa kumaliza elimu ya msingi mwaka 2024 utakaofanyika Septemba 11 mpaka 12 ambapo wanafunzi watakaofanya mtihani katika wilaya hiyo ni 5576, wavulana 2634 na wasichana 2942. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Serikali yataja faida wanaohama Hifadhi ya Ngorongoro

**Na Godfrey Mushi,** NGORONGORO

SERIKALI imesema mwitikio uliopo sasa wa wananchi kuendelea kuhama kwa hiari ndani ya eneo la Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA), kunasaidia kupunguza shughuli za kibinadamu hifadhini.

Pia inasaidia kukosa uhuru wa kumiliki vyombo vya moto, kufanya shughuli za kiuchumi pamoja na kukosa uhuru wa kutembea ndani ya hifadhi baada ya saa 12 jioni.

Katibu Tawala wa Wilaya ya Ngorongoro, mkoani Arusha, Hamza Hussein, alisema hayo wakati akizungumza na kaya 58 zenye wananchi 228 za jamii za kifugaji za kimasai.

Alisema jambo kubwa zaidi kuhama kwao kunasaidia kupunguza shughuli za kibinadamu hifadhini.

Wananchi hao waliagwa jana kwa ajili ya kuelekea Kijiji cha Msomera, Wilaya ya Handeni (Tanga) na maeneo mengine waliyochagua katika Wilaya za Monduli (Arusha), Meatu (Simiyu) na Simanjiro (Manyara).

"Tunawapongeza kwa uamuzi wa kuhama hifadhini, kwa ajili ya kupisha shughuli za uhifadhi, maeneo mnayohamia serikali imeshawajengea huduma muhimu kama shule, zahanati, maji, majosho, mawasiliano, nishati ya umeme, makazi bora pamoja na mashamba ya kilimo na malisho," alisema na kuongeza:

"Niwahakikishie wananchi ambao bado hawajaamua kuhama, kuwa serikali itaendelea kutoa huduma za kijamii na katika utekelezaji wa zoezi hili, tutaendelea kuzingatia misingi ya sheria, kanuni, taratibu na haki za binaadamu." alisema

Meneja mradi wa kuhamisha wananchi wa Ngorongoro, Ofisa Uhifadhi Mkuu, Flora Assey, alisema kundi hilo la 19 la awamu ya pili, limehamisha pia mifugo 350 ya wafugaji hao kwenda katika ardhi wanayohamia.

"Kati ya kaya 58 zilizohama leo (jana), kaya 30 zenye watu 151 na mifugo 235 zinahamia Kijiji cha Msomera, Kaya 28 zenye watu 78 na mifugo 115 zinakwenda maeneo mengine waliyochagua katika Wilaya ya Monduli mkoani Arusha, Meatu mkoani Simiyu na Simanjiro katika Mkoa wa Manyara," alisema.

Zaidi alifafanua: "Tangu zoezi la kuhamisha wananchi kwa hiari lilivyoanza Juni 2022 hadi kufikia Septemba 7, 2024 Jumla ya kaya 1,627 zenye watu 9,778 na mifugo 40,051 zimeshahama ndani ya hifadhi ya eneo la Ngorongoro."

Mmoja wa waliohama, Elizabeth Saiboko, Mkazi wa Kijiji cha Nainokanoka, alisema ameamua kuhama ndani ya hifadhi, ili kuwa huru zaidi na kutafuta kesho iliyo bora kwa watoto wake.

Alisema katika Tarafa ya Ngorongoro sheria za uhifadhi zinazuia baadhi ya shughuli za kiuchumi kama kilimo na ujenzi wa nyumba za kudumu.

# Rutazaa afichua kiini kufa vikundi vingi vya vikoba

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

MKURUGENZI Mtendaji wa Shirika la Maendeleo ya Jamii la Tusonge (CDO), Aginatha Rutazaa, amesema vikundi vingi vya wanufaika wa mikopo ya asilimia 10 vinakufa kwa sababu vinapoingia kwenye muunganiko, maslahi binafsi yanatawala zaidi na kumeza maslahi ya kikundi.

Alisema hayo katika Kata ya Majengo, Manispaa ya Moshi mkoani Kilimanjaro, wakati wa kuvunja mzunguko wa 16 wa kikundi cha Amkeni Vicoba Group.

Aginatha alisema chanzo kikubwa cha kufa vikundi vingi, ni matumizi ya ovyo ya wanachama kukosa nidhamu ya fedha.

"Ukichunguza matumizi ya siku ya wanachama wengi ni matumizi ya ovyo. Mgeni amekuja nyumbani kwake anakimbilia kumuuliza unakunywa soda gani, kwani mgeni kakwambia umnunulie soda?," alisema na kuongeza:

"Unaingia kwenye matumizi yasiyo sahihi, nidhamu ya fedha ni pamoja na kujizuia kufanya vitu ambavyo ukiviangalia mbele havina matokeo. Sio kukufaidisha tu wewe, matokeo ya kufaidisha pia familia yako na jamii kwa wigo wake".

Zaidi aliongeza, "Nidhamu ya fedha ni kitu muhimu na ndiyo siri ya mafanikio. Watu waliojenga maghorofa, wenye kampuni kubwa, wenye maisha ya kufuru, ni watu walioanza na mtaji wa Sh. 10,000 hadi Sh. 20,000, wauza karanga, wapiga viatu rangi waliokuwa na nidhamu ya fedha. Leo hii wenye kampuni kubwa walioajiri watu na wanaoweza kupata kipato kikubwa ambacho kinasaidia serikali yetu na kusaidia ustawi wa Tanzania".

Mwenyekiti wa Amkeni Vicoba Group, Grace Komba, alisema kikundi hicho kilichoasisiwa na Shirika la Tusonge CDO, mpaka sasa kimefikisha mtaji wa Sh. milioni 62.5.

Kabla ya kutoa taarifa hiyo, kikundi hicho kilifanya matendo ya huruma kwa kupeleka misaada ya kibinadamu katika kituo cha kulea watoto wenye mtindio wa ubongo na wenye ulemavu wa viungo cha BCC Majengo, kinachohudumiwa na Dayosisi ya Kaskazini ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT).

Aidha, Diwani wa Kata ya Majengo, Humphrey Mosha, alikipongeza kikundi hicho kwa kuwa kinara wa mafanikio ya kiuchumi kati ya vikundi vyote vya wanufaika wa mikopo ya asilimia 10 vilivyoko katika Manispaa ya Moshi.





# Tanzania kuwa kitovu teknolojia mawasiliano Afrika

**Na Maulid Mmbaga**

WADAU wa mawasiliano nchini wamesema mazingira imara na wezeshi yanayoendelea kuwekwa na serikali kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), yamekuwa kichocheo kikubwa cha kuwafanya wafikie malengo ya kuiwezesha Tanzania kuwa kitovu cha teknolojia ya mawasiliano Afrika.

Akizungumza na waandishi wa habari jana mkoani Dar es Salaam, Mkurugenzi wa Mawasiliano wa kampuni ya Airtel Tanzania, Beatrice Singano, alisema katika nchi nyingi ambazo ziko Afrika Mashariki, Tanzania ndiyo inayoongoza kwa kuwa na kiwango kikubwa cha teknolojia ya mawasiliano.

Alisema katika ukanda huu pia ni Tanzania pekee ndiyo yenye utaratibu unaoziruhusu kampuni za mawasiliano zilizo na leseni kuendesha teknolojia yoyote, tofauti na mataifa mengine ambayo mtu akitaka kutoka kwenye intaneti ya kasi ya 3G kwenda 4G ni lazima aombe leseni upya.

"Serikali imetuwekea utaratibu wa kutengeneza leseni ambayo inaakisi teknolojia yoyote bila kuwa na changamoto ya kutaka kupata ridhaa unapotaka kuhama kutoka teknolojia moja kwenda nyingine, tunashukuru mamlaka kwa mazingira haya mazuri na tunaamini tutaendelea kufanya biashara kwa ufanisi," alisema Beatrice.

Alisema mkongo wa mawasiliano wa baharini wa 2Afrika unaomilikiwa na kampuni hiyo, ambao ulizinduliwa na Rais Samia Suluhu Hassan mwaka jana umekuwa chachu katika kukua kwa kasi ya intanenti na kuongeza ufanishi wa mawasiliano nchini.

Alisema mkongo huo ambao kitovu chake ni Tanzania utahudumia mataifa zaidi ya nchi 40 za Afrika, na kwamba umesaidia kuifungua nchi, kuwezesha mikakati ya serikali ya kukaribisha wawekezaji na kuwasaidia Watanzania kurahisisha mchakato mzima wa huduma zinazotolewa kwa kutegemea intaneti.

"Mkongo huu wenye ukubwa wa zaidi ya kilometa 45,000 pia unaunganisha mabara matatu Afrika, Asia na Europe, ni kati ya miundombinu muhimu sana ambayo inatoa mawasiliano na kupeleka katika mataifa mbalimbali, na utaongeza pato la nchi kutokana na biashara itakayofanyika," alisema.

Alisema Tanzania kuna intaneti ya 5G ambayo imetokana na jitihada mbalimbali zinazofanywa katika kuinua sekta ya mawasiliano nchini, akieleza kuwa ni imani yao kwamba wanavyozidi kusonga mbele na kupata mifumo inayorahisisha mawasiliano, gharama pia zitapungua kutokana na matumizi yanavyoongezeka.

# Kampeni maalum ya kuwalinda watoto yazinduliwa

**Na Ada Ouko,** MUSOMA

JESHI la Polisi mkoani Mara, limezindua kampeni maalum ya kuwalinda watoto dhidi ya vitendo vya unyanyasaji na ukatili wa kijinsia. Akifungua kampeni hiyo juzi, Mrakibu Mwandamizi wa Polisi kutoka Dawati la Jinsia, Edison Mwamafupa aliwataka watoto hao kutokubali kurubuniwa wala kutofumbia macho vitendo vya ukatili ambavyo vinahatarisha na kukatisha ndoto zao.

"Vitendo kama ulawiti, ubakaji, utumiaji wa dawa za kulevya vyote hivi ni kinyume na sheria za nchi adhabu yake ni kifungo cha miaka 30 jela," alisema Mwamafupe.

Aidha, alitoa wito kwa wanafunzi hao kutoa ushirikiano kwa jeshi hilo punde wanapohisi viashiria hama wanapokumbwa na vitendo hivyo na kutoa taarifa kwa wazazi, walimu na viongozi wa dini.

Mkuu wa dawati hilo, Herieti Tagata alisema kumekuwa na tabia ya baadhi ya wananchi kumaliza kesi za ukatili kimya kimya kwa kulipana fidia na kuwaficha washukiwa wa vitendo hivyo, jambo ambalo linachangia ongezeko la vitendo hivyo katika jamii.



Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii ikikagua mradi wa ujenzi wa kituo cha utoaji taarifa kwa wageni wakati wa ziara ya kikazi ya kamati hiyo ya kukagua miradi iliyo chini ya ya Mradi wa Kuboresha Usimamizi wa Maliasili na Kukuza Utalii Kusini mwa Tanzania (REGROW) katika Hifadhi ya Taifa Ruaha, Mkoani Iringa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

# Wananchi 25,414 wanufaika na mradi wa maji Kahama

**Na Shaban Njia**, KAHAMA.

WAKAZI 25,414 wa Kata ya Mwendakulima Halmashauri ya Manispaa ya Kahama, wameondokana na adha ya upatikanaji majisafi na salama baada ya kampuni ya Napol Group kama sehemu ya kurudisha kwa jamii.

Wakieleza adha walizokuwa wakikumbana nazo kabla ya kufikiwa na huduma hiyo baadhi ya wakazi hao akiwemo Rehema Juma, alisema awali walikuwa wakichota maji kwenye madimbwi na visima walivyochimba wao wenyewe.

Mkazi mwingine, Suzana Mpenzu alisema walikuwa wakitumia maji sehemu moja na mifugo yao, kutumia katika kilimo cha mboga (bustani) hali iliyokuwa ikisababisha kuwepo kwa mlipuko wa magonjwa ya mara kwa mara.

Diwani wa kata hiyo, Abrahman Manyelo alikiri kuwepo kwa adha ya upatikanaji wa maji hali inayosababisha kutumia maji yasiyosafi na salama, hivyo kuahidi kulinda mradi huo wa maji yaliyochimbwa na kampuni hiyo ambayo yanatumiwa bure na wananchi.

Ofisa Masoko na Uhusiano kutoka Napol Group of Company, Eliphidas Mushi alisema wanatambua umuhimu wa huduma za kijamii na ndiyo sababu ya kuwafikishia wananchi huduma ya maji, sehemu ya faida wanayoipata kupitia uzalishaji wanaoufanya na kuwaondolea adha ya ukosefu wa maji safi na salama.

Alisema huduma hiyo itakuwa inatolewa bure kwa wananchi bila ubaguzi, itakuwa inaanza saa kumi na mbili asubuhi mpaka jioni.

# Tril.5/- kuwekezwa uchimbaji nickel Ngara

**Na Judith Julius,** NGARA

ZAIDI ya Sh.trilioni 5.45 zinatarajiwa kuwekezwa katika mradi wa uchimbaji madini aina ya nickel wilayani Ngara mkoani Kagera.

Hayo yalibainishwa juzi na Waziri wa Madini, Anthony Mavunde, alipofanya mazungumzo na viongozi wa kampuni ya madini ya BHP inayotarajia kuingia ubia na kampuni ya Lifezone Metal kufanikisha uwekezaji huo nchini.

Alisema mazungumzo hayo yalijikita katika kutoa taarifa ya maendeleo ya mradi wa Kabanga Nickel unaosimamiwa na kampuni ya ubia ya Tembo Nickel ambayo serikali pia ni mwanahisa.

"Mradi wa Kabanga Nickel unatarajiwa kugharimu kiasi cha zaidi ya Dola za Marekani bilioni mbili ambako zaidi ya Dola bilioni 1.6 zitatumika kwa ajili ya shughuli za ujenzi wa mgodi na uchenjuaji wa madini utakaofanyika wilayani hapa," alisema Mavunde.

Kadhalika alisema zaidi ya Dola za Marekani milioni 500 zitatumika kwa ajili ya ujenzi wa kiwanda cha usafishaji wa madini kitakachojengwa katika ukanda maalum wa kiuchumi eneo la Buzwagi wilayani Kahama mkoani Shinyanga.

Kampuni ya BHP ni moja kati ya kampuni kubwa tatu za madini duniani ambayo ina mapato ya Dola za Marekani bilioni 60 kwa mwaka sawa na Sh.trilioni 160. Kampuni hiyo inayotazamia kuingia makubaliano ya ubia na kampuni ya Life Metals kuendeleza mradi wake Kabanga, ilifunga shughuli za uchimbaji madini Afrika miaka 15 iliyopita na sasa ipo tayari kurejea Afrika kupitia uwekezaji wake nchini.

Waziri Mavunde aliishukuru kampuni hiyo kwa kuiamini Tanzania na kuamua kurudi kuwekeza kupitia mradi wa Kabanga, huku akiwahakikishia mazingira mazuri ya uwekezaji.

Alisema hatua hiyo ni mwendelezo wa mipango ya serikali kuvutia uwekezaji nchini kwa kutengeneza mazingira wezeshi kwa wawekezaji.

Mavunde, ambaye aliongozana na Balozi wa Tanzania nchini Japan, Baraka Luvanda, ambaye pia anasimamia Australia walishuhudia teknolojia itakayotumiwa kwenye ujenzi wa kiwanda cha kusafisha madini ambayo itatumia teknolojia ya kisasa ya Hydrometallurgy.

Nipashe
# TESA
Jumanne Septemba 10, 2024
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI






Ukurasa 12

Mara mbioni kutumia sheria ndogo kufanikisha wanafunzi kupata mlo



Ukurasa 14

Mbunifu wa bendera ya Nigeria anayeishi 'mochwari' mwaka mzima

**NA JULIETH MKIRERI, KIBAHA**

FAMILIA WATU 6 WASIOONA

# Wanapomwangukia Rais Samia awashike mkono

- Wadai kutengwa, wanaitwa wachawi, hawamudu hata mlo mmoja wa siku

WATANZANIA wanafuatilia mambo mengi anayofanya Rais Samia Suluhu kwa taifa, lakini hata kwa mtu mmoja mmoja. Mfano ni ahadi ya kumsomesha na kujengea makazi familia ya mtoto Alhaj Abdallah na mama yake mjane wanaoishi Kigoma.

Aidha, Rais anagharimia matibabu ya upasuaji na utengamano kwa watoto 100 wenye vichwa vikubwa na mgongo wazi, kazi ikifanyika katika Taasisi ya Tiba ya Mifupa na Ubongo Muhimbili (MOI).

Vivyo hivyo, hata familia yenye historia ya kusisimua lakini inayoleta uchungu, ya mama Mwajuma Maulid (70), yenye watu wengi wasioona, inatamani mkono wa Rais awaguse na kuwaondolea simanzi na huzuni ya kukosa hata chakula.

Ikizingatiwa Rais Samia ni mama na mlezi anayeguswa na changamoto kama hizo na kuwashika mkono wengi, mara hii familia ya Mwajuma, inafikisha kilicho chao kupitia gazeti hili.

Kila anayeiona familia hiyo huenda anajiuliza hivi ni nani anayeweza kuwabeba Watanzania hawa?

Nyumbani kwao ni takribani kilometa tatu kutoka Barabara Kuu ya Morogoro katika kituo cha daladala cha Kibaha Kwamfipa mkoani Pwani.

Wanaishi mtaa wa Simbani, ndani ya familia hiyo ya watu 25 kati yao wasioona ni sita.



Mwajuma Maulid (kulia) na familia yake watoto na wajukuu nyumbani kwake Simbani wilayani Kibaha. **PICHA:JULIETH MKIRERI**

Mkuu wa kaya ni mama Mwajuma Maulid aliyebarikiwa kuwa na watoto sita akiwa na mumewe Nasoro Likame (85). Wakike ni watano na mwanaume mmoja, anaiambia Nipashe.

Baba yao pia haoni na katika watoto hao sita wanne hawaoni na wawili wanaona.

Mwajuma anaeleza kuwa, mumewe alimkimbia akamuachia watoto wote sita ambao alipambana mchana na usiku kuwalea akifanya kazi za vibarua na kilimo ili kupata chakula na mahitaji.

Anasema si ndugu wa mume, majirani wala yeyote ambao wanaguswa na familia hiyo wote kwa pamoja wameitenga na kuacha malezi yote kumuangukia akiwahudumia kwa kila kitu.

**MAISHA YA FAMILIA**

"Familia ilinitenga. Sina msaada kutoka kwa ndugu wa mume wanadai nimezaa sana, hata majirani hawashughuliki na mimi wanadai ni mchawi ndiyo sababu wanangu wako hivi nimeamua kusimama mwenyewe na Mungu kwenye malezi yao," anasema.

Mwajuma anaelezea kwamba watoto wake wote bila kujali wanaoona na wasioona aliwafundisha kazi zote za nyumbani kupika na pia kufuata maji mtaa mwingine ambapo ni zaidi ya mita 100 kutoka wanapoishi.

Ukweli ni kwamba, si kawaida kwa watu ambao hawaoni kutembea wenyewe bila msaada wa mtu au fimbo nyeupe, haijazoeleka lakini kwa wanafamilia hao wanatembea bila fimbo hawashikwi mkono na kustaajabisha zaidi.

Mama huyo anasema bila kuwafundisha hivyo wasingemudu kumsaidia kazi, ikiwa anaumwa au ametoka nyumbani.

"Wanangu hawa pia wamekuwa wakifanya vibarua kulima kwenye mashamba ya watu wananisaidia tunapata fedha za kununua chakula na mahitaji, "anaeleza.

Anasema watoto hao hawakusoma kutokana na umbali wa shule na kukosa fedha za usafiri wa kila siku na vifaa vya usaidizi.

Anasema hata kwa upande wa wajukuu yupo ambaye ameishia kidato cha pili kutokana na kukosa mahitaji na vifaa vilivyokuwa vinatakiwa shuleni na hivyo kuendelea kubaki nyumbani huku mwingine mdogo wake wa miaka tisa naye akishindwa kuanza masomo.

Leila Nasoro (48) ni mtoto wa kwanza katika familia ya Mzee Nasoro na Mwajuma ambaye pia haoni. Mama huyo ana watoto watano, wawili hawaoni.

"Mbali ya kulima vibarua tunashona mikeka na mama anatutafutia wateja kuiuza na kupata fedha za kujikimu." Anasema Leila.

"Pamoja na hali yangu hii ninachoma mkaa ninasaidiwa na mdogo wangu ambaye anaona, nalima mpunga pia nikivuna chakula, hapa nyumbani tunamsaidia mama kutokana na familia kubwa aliyonayo," anasema Leila.

Mbali na kutengwa na jamii kutokana na kuwa na familia kubwa yenye watu wasioona hata wakienda serikali za mitaa kupata huduma ushirikiano ni

INAENDELEA UK.14

ELIMU

## NA SABATO KASIKA CHAKULA SHULENI

# Mara mbioni kutumia sheria ndogo kufanikisha wanafunzi kupata mlo

"KUCHANGIA kilo moja ya unga na ya maharage kwa mwezi kwa mtoto wako anayesoma shule ya msingi au sekondari kunabadilisha maisha yake shuleni na kumpa uhakika wa elimu bora, kuliko kumuacha na njaa."

Mkuu wa mkoa wa Mara, Kanali Evans Mtambi, akiangalia mahitaji hayo anatoa ujumbe huo mahsusi kwa wazazi, walezi na wadau wa elimu kuwapatia wanafunzi chakula shuleni.

Akizungumza na viongozi wa Chama cha Wakuu wa Shule za Sekondari (TAHOSA) mkoani humo katika kikao cha mwaka anawataka kusimamia utekelezaji wa mpango wa kulisha watoto shuleni.

Anaelekeza kuwa ni lazima wanafunzi wote katika shule zao wapate chakula cha mchana wawapo shuleni, lakini pia anawataka wazazi na walezi kutimiza wajibu kuwapa watoto chakula.

Akizungumza katika kikao hicho, anaagiza kuwa kama Nipashe Kanali Mtambi anasema, kama kuna matatizo yanayokwamisha utaratibu huo, wakuu wa shule wayawasilishe kwa viongozi wa maeneo yao, ili yapatiwe ufumbuzi, akisisitiza wanafunzi kupata chakula.

"Mkoa wa Mara hakuna mwanafunzi atakayeshinda njaa kwa kuwa mzazi au mlezi wake hataki kutimiza wajibu wake wa kumpatia chakula, tutawachukulia hatua za kisheria," anasema Kanali Mtambi.

Anapiga marufuku shule kutoa chakula kwa baadhi ya wanafunzi na kuwaacha wengine, kwa sababu wazazi au walezi hawajachangia , badala yake wakuu wa shule watoe taarifa kwa viongozi wa serikali katika maeneo yao ili wachukulie hatua za kisheria.

"Sitakubali ukatili huu kwa wanafunzi uendelee eti kwa sababu wazazi na walezi hawataki kuchangia chakula kwa ajili ya watoto wao kula shuleni mchana. Wakuu wa shule toeni taarifa kwa viongozi wa serikali kuhusu wazazi wote ambao wamekataa kutimiza wajibu wao wa kutoa chakula cha watoto wao," anasema.

Aidha, anawataka wakuu hao wa shule za sekondari wajenge majiko na stoo kwa kufuata maelekezo ya taasisi ya Pamoja Tuwalishe ili shule zote mkoani humo ziweze kupatiwa majiko banifu na sufuria zake ili kuleta uhakika wa wanafunzi wengi kupata chakula cha mchana shuleni.

Kaimu Katibu Tawala Msaidizi Elimu na Mafunzo ya Ufundi,



Mkuu wa Mkoa wa Mara, Kanali Evans Mtambi akizungumzia umuhimu wa chakula shuleni. **PICHA ZOTE: MPIGAPICHA WETU**

Makwasa Bulenga anawataka wakuu hao wa shule kutekeleza maagizo ya Katibu Tawala wa Mkoa wa Mara, Gerald Kusaya aliyotoa wakati wa ufunguzi wa kikao hicho.

"Mnaporudi katika vituo vyenu vya kazi baada ya kikao hiki muoneshe mabadiliko, katika usimamizi wa shule zenu, hasa ujifunzaji na ufundishaji wa wanafunzi na walimu," anasema Bulenga.

Bulenga anawataka wakuu wa shule ambao hawakuhudhuria kikao hicho kutoa maelezo yao kuhusu sababu zilizowafanya kuacha kushiriki katika kikao hicho ambacho anasema kilikuwa muhimu kwa wakuu wote.

**KUHAMASISHA WAZAZI**

Mkuu wa Shule ya Sekondari Kirumi, Anna Sarita, anasema kwa niaba ya walimu wenzake kuwa watakwenda kutumia bodi za shule kuhamasisha wazazi na walezi kuchangia chakula.

"Lakini pia tutakwenda kutumia majiko banifu ili wanafunzi waweze kupikiwa chakula katika mazingira safi na salama na bila kuharibu mazingira," anasema Anna.

Mwalimu huyo anasema, wapo baadhi ya wazazi na walezi ambao hawaelewi umuhimu wa chakula cha watoto wao shuleni, huku wengine wakikataa kuchangia kutokana na sababu wanazozijua wenyewe.

"Ni wajibu wetu kuongeza kasi katika kuwafuatilia wazazi na walezi ili wachangie chakula cha watoto wao na kama watatokea wakorofi, tutatoa taarifa kwa uongozi wa serikali za mitaa," anasema.

Anna anasema, uelewa mdogo wa jamii juu ya utoaji wa chakula katika shule, baadhi ya wazazi walezi bado wana dhana kuwa kuchangia chakula shuleni ni kupoteza fedha," anasema.

Mwalimu huyo anaongeza kuwa wengine wanaamini kuwa utoaji wa chuakula shuleni ni jukumu la serikali, kwa kuwa ilishatangaza kutoa elimu bure, hivyo, inatakiwa pia kutoa chakula

Anasema, wengine wanaamini kuwa mwanafunzi kurudi nyumbani kula ndiyo njia rahisi zaidi, bila kuangalia kujali kwamba mtoto anaishi mbali kiasi gani na shule au karibu na shule.

"Hivyo, tutatumia mbinu ya kuitisha vikao vya wazazi, walezi na wazee maarufu,bodi za shule kwa kushirikisha viongozi wa vijiji au mitaa ili kutoa elimu kwa wazazi juu ya umuhimu wa chakula shuleni," anasema.

**HAKUNA CHAKULA**

Karibu shule zote zinakabiliwa na tatizo la ukosefu wa chakula, unaotokana na baadhi ya wazazi na walezi kutotekeleza agizo la serikali la kuwataka wachangie.

Hali hiyo inawasukuma wadau wa elimu kushauri kwamba ziundwe sheria ndogo za halmashauri ili kuwabana wale wanaokwepa kuchangia ili waweze kutimiza wajibu kikamilifu.

Ushauri huo umewahi kutolewa na wajumbe wa Kamati ya Lishe Wilaya ya Gairo mkoani Morogoro, katika kikao cha kamati hiyo cha kujadili taarifa za hali ya lishe shuleni baada ya kuona baadhi ya wazazi na walezi hawachangii chakula kwa ajili ya watoto wao.

Wanaamini kuwa njia hiyo itawabana wote wanaokaidi agizo la chakula shuleni ambalo pia linalenga kupunguza utoro wa baadhi ya wanafunzi wanaoshindwa kufika shuleni kwa kuhofia kushinda njaa.

Katika mchango wake kwa niaba ya wakuu wa idara za elimu msingi na sekondari, Ofisa Habari Mawasiliano na Uhusiano Wilaya ya Gairo, Cosmas Njingo, anasema ipo haja ya idara hizo kuweka mkakati wa kutunga sheria ndogo za kuwabana wazazi na walezi wanaokaidi agizo la serikali la kuwataka kuchangia chakula ili kuwawezesha watoto wao chakula cha mchana shuleni.

"Ushauri wangu kwa idara hizi mbili, zianzishe mchakato kupitia Ofisi ya Ofisa Sheria wa halmashauri wa kuandaa rasimu ya sheria ndogo za kuwabana wazazi na walezi wanaokaidi kwa makusudi agizo halali la serikali linalowataka kuchangia chakula shuleni kwa ajili ya watoto wetu," anasema Cosmas.



Wakuu wa sekondari wakifuatilia kikao hicho.

ELIMU

NA GAUDENSIA MNGUMI

SIMULIZI LA UKWELI

# Kusaka utajiri chapchap kulivyomponza msanii akizikwa hai, anusuriwa mahututi

• Mganga tapeli akisimamia mchakato porini, baada ya kula hela atokomea

KATIKA jitihada za kufikia mafanikio ya kimuziki kwa kasi, vijana wanapitia changamoto nyingi na mojawapo ni kurubuniwa na wajanja wanaojiita waganga wataalamu wa kufanikisha biashara.

Akisimulia kisa cha kurubuniwa na aliyejiita mleta mafanikio, Salimu Mbasha maarufu kama Rupia Boy, anasema mwaka 2022, baada ya kurekodi nyimbo kadhaa, alishauriwa na marafiki kutafuta njia mbadala ya kupata mafanikio ya haraka.

"Tulianza kazi kwa kurekodi kwenye studio (jina tunalo) ya Dar tulikutana na wasanii wenzetu waliotupa namba , akatuambia ili kuwa 'supa staa' uje tukutengeneze . Nikatajiwa gharama karibu Shilingi 1,000,000."

Rupia anasema lilikuwa dau kubwa akalazimika kufanya maarifa akiuza mali za bibi yake na kumpelekea mganga alichotaka. Ili afanikiwe alitakiwa kuingizwa kwenye jeneza na kuzikwa ardhini kwa siku mbili akifukiwa na udongo .

"Tulikutana Sinza kwenye eneo moja la burudani. Baada ya majadiliano na kulipa tuliondoka Dar es Salaam kwenda Iringa kwenye msitu ambao siufahamu. Tuliondoka usiku akiendesha gari lake binafsi. Tulifika sehemu akanionesha jeneza na kila kitu kilikuwa kimeandaliwa." Anasema Rupia.

Anaeleza kuwa, kabla ya kufika mganga alikuwa amewasiliana wa wenyeji wao na ilikuwa ni kufika na 'kutibiwa'.

Anasema kabla ya kuingia kwenye jeneza la mbao analosema ni linalotumiwa na Wakristo, alichomwa sindano kwenye mshipa mkuu wa mkono wa kushoto, akashtuka.

Anaeleza kuwa, hospitali damu ya mshipa huo hutumiwa kuchunguza magonjwa kama typhod, homa ya manjano au kwa kitaalamu vipimo vya 'full blood picture'

Mganga alimwambia kuwa akifukiwa atakuja kumfukua baada ya siku mbili, na kwamba alifukiwa Ijumaa saa 9 usiku hivyo, angemfukua tena Jumapili saa 9 usiku pia.

Rupia, anasema aliingiwa na wasiwasi, katika safari hiyo aliyokuwa ameambatana na marafiki zake watatu (majina tunayo), akiwaambia, ukifika wakati huo kama mganga huyu, hajamfukua, wamfukue.

"Hata kama itakuwa nimepoteza maisha wafahamisheni wazazi na ndugu zangu hasa mama mzazi na bibi aliyenilea."

Anaeleza kuwa, baada ya kuchomwa sindano hiyo alipoteza fahamu na kuona giza na hakufahamu kilichoendelea tena.

"Nimekaa kaburini siku ya kwanza ya pili haikuisha. Marafiki zangu wakawa wanawasiliana na mganga lakini hakupokea simu na hakupatikana tena mpaka leo. Licha ya kwamba namba yake awali ilikuwa inatumika hadi tulipofika kwenye kaburi msituni."



Rupia

**KUZIKWA**

Msanii huyo anasema halikuwa kaburi refu kwenda chini lakini pengine lilikuwa na mita moja na nusu , hivyo haikuwa kazi ngumu marafiki zake kumfukua.

Anasema akiwa kaburini humo hakuona chochote mbali na kuzimia , akiamini kuwa mganga alikuwa amekusudia kumuua.

Hata hivyo, japo hakufahamu dawa aliyochomwa kwenye mshipa anahisi ilikuwa ni nusu kaputi kwa sababu ingekuwa sumu angetoa povu la damu mdomoni na sehemu zote za mwili zenye matundu.

**KUOKOLEWA**

Rupia anasema marafiki zake hawakuondoka Iringa, walisubiria lakini walipoona mganga ametokomea, hapatikani tena, walikuja kumuokoa Jumamosi usiku na kufukua kaburi na kumkuta akiwa mahututi.

Wanamueleza kuwa alikuwa hajitambui na kupelekwa hospitali binafsi na kutibiwa kwa kuwekewa drip za kuondoa sumu mwilini, kuongezewa sukari na maji.

"Nililazwa hospitalini siku mbili hadi bibi na mama wakitokea mikoani walipofika kunichukua na kuendelea na tiba na huduma nyingine kutoka kwenye familia."

Akisimulia alivyokutana na mganga huyo feki, Rupia anasema kimuonekano anaonekana baba wa makamo na anajitambulisha kwa jina la Shekhe Sanga.

Hata hivyo, anasema licha ya kupoteza fedha nyingi hakufanikiwa wala hajafahamu mganga huyo yuko wapi ila ana wasiwasi wapo wasanii, Watanzania wengi ambao huenda wamepoteza maisha yao kwa udanganyifu huo.

Anawashauri wasanii,wajasiriamali na wengine wenye nia ya kupata mafanikio wasisikie chochote ama kwa kushauriwa au kwa kuelezwa na hata kuoneshwa kuwa kuna tabibu wa kuwapa mafanikio chapchap.

**KURIPOTI**

Anasema walifikisha mkasa huo kituo cha polisi Oysterbay Dar, lakini ilikuwa vigumu kupata mawasiliano na mtuhumiwa lakini pia ushahidi wa kufanyika kwa tukio hilo Iringa haukuwapo.

Anawashauri vijana kuwa makini na masuala ya kutumia njia mbadala (short cut) kupata mafanikio, hasa kupitia waganga wa kienyeji.

Anasema Watanzania pia wawe makini na matangazo ya waganga yanayotolewa popote mitandaoni na mitaani, kwenye mabango au matangazo yanayobandikwa kwenye nguzo za umeme kwa sababu ni uongo lakini pia ni wauaji.

"Kama marafiki zangu wasingekuwapo inamaana ningekufa na hakuna mtu angejua taarifa zangu. Lakini pia kama ningekuwa peke yangu angeweza kunimaliza kwa sindano hizo anazochoma wateja wake. Inawezekana pia ukachomwa sindano ya sumu ni lazima kuwa makini sana nyakati hizi."

Rupia anasema matapeli ni wengi na wanajua kuwa watu wana njaa ya utajiri na mafanikio ya haraka hivyo wanafanya wapendavyo.

"Wanaweza kukutajia kiasi cha fedha wanachotaka hata milioni 10. Baadhi ya vijana wanalazimika kuiba kumbe wanaambulia kifo na zaidi kujiongezea umaskini." Anaonya Rupia.

**ANACHOFANYA**

Baada ya heka heka hizo msanii huyo mzaliwa wa Mwanga mkoani Kilimanjaro, alisimama kwa muda na sasa amerudi tena kwenye muziki na hivi karibuni aliachilia kibao kipya anachokiita Zigo.

***FUATILIA WIKI IJAYO WANAYOSIMULIA WAZAZI NA MARAFIKI .**

ELIMU

NA MWANDISHI WETU

# Mbunifu wa bendera ya Nigeria anayeishi 'mochwari' mwaka mzima

## • Akumbukwa, sasa kuzikwa wiki hii

FAMILIA ya mwanamume aliyebuni bendera ya Nigeria inakata tamaa kusubiri mazishi ya kiserikali iliyoahidiwa, ukitimia mwaka mmoja sasa.

Ni baada ya kifo cha jamaa yao, mbunifu wa alama kuu ya taifa hilo.

Mbunifu Taiwo Michael Akinkunmi (87), aliyefariki mwaka jana, atazikwa wiki hii nyumbani kwake katika jimbo la Oyo.

Akinkunmi, anayejulikana na wengi kama "Mr Bendera " au Bwana Bendera, nyumba yake ilipakwa rangi ya kijani kibichi na nyeupe rangi za bendera ya taifa hilo.

Anaelezwa kuwa alikuwa mnyenyekevu, na

mwanae anatumaini wakati wa mazishi yake , ambayo jimbo la Oyo limekubali kuyagharamia, atakumbukwa kwa ubunifu. Anasema ubunifu huo ni ishara ya umoja wa Nigeria.

Tunapaswa kumpa mazishi yanayostahili," mwanaye Akinwumi Akinkunmi anasema kwenye kipindi cha BBC Focus on Africa.

Anaongeza kuwa alikuwa mbunifu wa bendera asiyetarajiwa. Aliingia katika shindano la kubuni bendera mpya kabla ya Nigeria kupata uhuru kutoka kwa Uingereza Oktoba 1960.

Wakati huo alikuwa akisomea uhandisi umeme jijini London na alikuwa ameona tangazo la gazeti kuhusu shindano hilo.

Kulingana na mtaalam wa bendera Whitney Smith, mapendekezo ya mitindo 3,000 ya bendera yaliwasilishwa "mingi ikiwa ni yenye utata mkubwa".

Lakini ubunifu wa Akinkunmi ulikuwa ni rahisi, alipendekeza bendera yenye milia ya wima yenye rangi za kijani, nyeupe, kijani na ubunifu ukichukua nafasi ya bendera ya kikoloni iliyokuwa na alama ya jeki ya muungano wa Uingereza na nyota ya kijani yenye ncha sita chini ya duara jekundu.

Ubunifu wa muundo wa asili wa Akinkunmi ulijumuisha jua jekundu lililozungukwa na miale katikati ya bendera.

Hii ilikusudiwa kama "ishara ya ulinzi na mwongozo wa Mungu", Smith anaandika katika Encyclopaedia Britannica, inasema BBC.

Hata hivyo, jua liliondolewa na kamati hiyo, ambayo ilimzawadia kijana Akinkunmi wakati huo akiwa na miaka 23 £100 zaidi ya Shilingi 300,000 kwa ushindi wa ubunifu wake wa bendera ya taifa.

Akinkunmi kila mara alisema msukumo wake ulitoka utotoni alipokuwa amesafiri na kuishi sehemu mbalimbali za Nigeria.

Akiwa mzaliwa wa Ibadan kusini-magharibi, ambao sasa mji mkuu wa jimbo la Oyo, aliishi miaka yake ya kwanza kaskazini mwa nchi wazazi wake walikokuwa wakifanyakazi.

Alikulia katika kile alichosema ni familia yenye furaha ya wake wengi na alikuwa mmoja wa watoto 10 wa baba yake.

Alirudi Ibadan kumalizia elimu yake. Aliwahi kumwambia mwandishi wa habari wa ThisDay Funke Olade, kwamba shule yake ya sekondari ilikuwa kama "Nigeria-ndogo" kwani ilikuwa na wanafunzi kutoka nchi nzima.

Nigeria ina makabila zaidi ya 300,wakati nchi hiyo yenye watu wengi zaidi barani Afrika haina dini rasmi.

Taifa hilo limegawanyika takribani kati ya eneo la kaskazini lenye Waislamu wengi na Kusini lenye Wakristo wengi, ingawa jamii nyingi zimechanganyika.

Kwa Akinkunmi rangi ya kijani kwenye bendera iliashiria urithi wa kilimo wa taifa, huku nyeupe ikiwakilisha amani na umoja.

"Ni kawaida kwa Nigeria, kama nchi nyingine zenye tamaduni nyingi kuchagua muundo rahisi wa bendera.

Muundo tata zaidi unaweza kuwa uliheshimu baadhi ya makabila na kuyatenga mengine," Smith aliandika.



Taiwo Akinkunmi. **PICHA: BBC**

Akinkunmi alipenda sana kilimo na alifurahi kurudi Nigeria baada ya uhuru kufanya kazi katika Wizara ya Kilimo, ambapo alikuwa mtumishi wa umma hadi alipostaafu mwaka 1994.

Lakini kwa muda mrefu wa maisha yake watu wachache walijua kuhusu mchango wake katika nchi, ingawa popote alipokuwa akiishi inasemekana alikuwa akipaka nyumba nye ya nyumba yake rangi za kijani na nyeupe.

Hakuwahi kutambulika hadi Nigeria ilioposherehekea mwaka wake wa 50 wa uhuru ndipo alipotambuliwa kama mmoja wa Wanigeria 50 mashuhuri.

Mwanaye anasema mwanasiasa wa jimbo la Oyo baadaye alishawishi apewe heshima ya kitaifa na pensheni na mwaka wa 2014 alipewa tuzo ya Ofisa wa Mamlaka ya Shirikisho la Jamuhuri (OFR), mojawapo ya tuzo za juu zaidi za Nigeria.

Baada ya kifo cha Akinkunmi mwaka jana, seneta mmoja alifadhili hoja iliyofaulu kwamba afanyiwe mazishi ya kitaifa.

Hata hivyo, hakuna mipango iliyowahi kufanywa na walipokuwa wakingoja, familia ya Akinkunmi imekuwa ikilipa naira 2,000 ($1.30; £1.00) kwa siku kuweka mwili kwenye chumba cha kuhifadhia maiti.

Mtoto wa mbunifu huyo wa bendera alisema kuwa mwezi Juni waligundua kuwa Taasisi ya Kitaifa ya Masuala ya Kitamaduni ya Wizara ya Sanaa (NICO) iliagizwa kushughulikia mazishi yake.

Lakini mbali na kupigiwa simu mara moja, alisema taasisi hiyo imeshindwa kuwasiliana zaidi na familia.

Anahisi kuchelewesha tena mazishi kungechafua jina la baba yake.

Hapo ndipo serikali ya jimbo la Oyo ilipoamua kuingilia kati kugharamia ibada ya mazishi ya mbunifu huyo wa bendera.

"Marehemu baba yangu alikuwa mtu mpole ambaye hakutaka chochote kumharibia sifa," mwanaye aliambia BBC.

# WANAPOMWANGUKIA RAIS SAMIA AWASHIKE MKONO

**INATOKA UK.11**

hafifu, anasema Leila.

Anaomba wadau mbalimbali kujitokeza kusaidia familia hiyo kwa misaada ya aina mbalimbali, ikiwemo chakula kwani kwasasa wanategemea zaidi mlo mmoja ambao ni kilo sita za unga kwa mlo mmoja.

"Hapa kwetu asubuhi tukibahatika kupata uji basi ni mpaka usiku uwezo wa milo mitatu hatuna tunaomba wanaoguswa watusaidie. Hatuoni lakini hatuwezi kukaa nyumbani tumtegemee mama peke yake na ndugu zetu wawili ambao si walemavu," anasema.

Mama na Leila wanaomba serikali iwashike mkono maana ndiyo pekee inayoweza kuwasaidia.

**AHADI ZA MSAADA**

Happiness Matagi mmoja wa viongozi wa kitaifa wa Chama cha Wasioona Tanzania, anasema wameshatembelea familia hiyo na wanaendelea kutafuta uwezekano wa kuwasaidia.

Anasema wataanza na mwanafunzi aliyekatisha masomo kwa kukosa mahitaji pamoja na mtoto wa miaka tisa aliyeshindwa kusoma.

Jabiri China Mwenyekiti wa Shirikisho la Vyama vya Watu wenye Ulemavu Tanzania (SHIVYAWATA), Wilaya ya Kibaha, anaahidi kumuita ofisini Leila ili kwa pamoja waandike barua kuomba kibali achangishe fedha kwa wahisani kupata mahitaji ya mtoto aliyekatisha masomo.

Anasema chama hakina fedha, wala ruzuku na hivyo kitu cha kusaidia kwa familia kama hiyo ni kuandika barua kwa Mkuu wa Wilaya kuomba kibali na kuwezeshwa, lakini pia kupata ruhusu ya kuchangisha fedha kutoka sehemu na watu mbalimbali.

Frazia Enos, Mratibu wa Watu Wenye Ulemavu Kitengo cha Ustawi wa Jamii Halmashauri ya mji wa Kibaha anasema suala la kunyanyapaliwa familia hiyo wanapokwenda kupata huduma kwenye ofisi za serikali watalishughulikia kujua ukweli.

Frazia pia anasema wanashirikiana na wadau mbalimbali kusaidia watu wenye ulemavu hivyo wataendelea kutumia utaratibu huo atakapopatikana mfadhili wa kuwahudumia.

Anazungumzia mikopo akisema utaratibu wa halmashauri kuanza kutoa mikopo ya asilimia 10 kwa wanawake asilimia nne, vijana nne pia na watu wenye ulemavu asilimia mbili utakapoanza wataiangalia familia hiyo.

"Leila pamoja na kaka yake waliwahi kunufaika na mikopo ya halmashauri, na utaratibu utakapotolewa wakiomba tutawapatia kwasababu mama yao amekuwa akiwasimamia kwenye biashara za mikeka wanayoshona na marejesho waliyafanya kwa ukamilifu hatuwezi kuwaacha," anaeleza Frazia.

Mratibu wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) Halmashauri ya Mji wa Kibaha Anita Lyoka, anasema kaya maskini na ya wahitaji ya Mwajuma itafuatiliwa kama haijaingizwa kwenye mpango wa kunusuru kaya masikini.

Hata hivyo, Lyoka anasema katika awamu ijayo utaratibu utakapotangazwa familia hiyo itapewa kipaumbele kuingizwa kwenye mpango huo ikibainika kama haijaibuliwa na wananchi.

Daktari wa macho Mkoa wa Pwani Dk.Eligreater Mnzavas, anasema zipo sababu zinazochangia kuleta upofu utotoni ambazo ni pamoja na mtoto wa jicho (cataract), presha ya macho pamoja na mtoto mdogo kutoka matongotongo au usaha anapozaliwa.

Dk.Mnzavas anasema matongotongo kuanza kutoka mapema mtoto akizaliwa, endapo atatibiwa mapema atakaona lakini iwapo hatapata tiba anapata upofu.

Anawakumbusha wazazi na walezi kuwa makini na watoto wachanga wanapoona dalili za ugonjwa wa macho.

Kadhalika anawakumbusha wengine kutibu macho na kuacha mazoea ya kupuuzia mtoto wa jicho au tatizo lolote.

Leila na mama yake wanaowaomba wanaoguswa na changamoto yao kufika nyumbani kwao Simbani kuona mazingira wanayoishi, mapungufu na matatizo yanayowazunguka ili waone namna bora ya kuwasaidia.



# Mavunde aanika mikakati kukomesha ukataji miti

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MBUNGE wa Dodoma Mjini, Anthony Mavunde ametaja mikakati mitatu ya kukabiliana na ukataji miti kwa ajili ya mkaa katika Halmashauri ya Jiji la Dodoma, mojawapo ni kuwakopesha vijana mitambo ya kutengeneza mkaa mbadala unaochakatwa kwa kutumia karatasi na taka.

Akizungumza jana jijini hapa kwenye mkutano maalum wa viongozi, wataalamu na wadau kuhusu mwenendo wa hali ya mazingira nchini, Mavunde alisema kuna vijana wengi wanaojishughulisha na biashara ya mkaa na ili kuwaondoa katika ukataji wa miti wamezungumza na Taasisi ya Uhandisi na Usanifu wa Mitambo nchini (TEMDO) mkoani Arusha ili kupata mitambo midogo kwa ajili hiyo.

Mavunde ambaye pia ni Waziri wa Madini, alisema mitambo hiyo itasaidia kuchakata magome ya miti, karatasi na uchafu mwingine kwa ajili ya kutengeneza mkaa ili kutatua tatizo la ukataji miti.

**"Kwasasa tupo kwenye mpango wa kuchimba visima ili kuhakikisha katika shule zote za msingi na sekondari zinahamasika kupanda miti na kutunza mazingira tunaanza hatua kwa hatua,"**

"Vijana hawa watakopeshwa kupitia asilimia 10 ya mapato ya ndani, tunaanza kuwakopesha vijana ili kupata mitambo hii midogo ya kutengeneza mkaa kupitia karatasi na uchafu mwingine na waache kukata miti ili tuyatunze mazingira," alisema.

Alitaja mikakati mingine ni kuweka sharti la lazima, kila kibali cha ujenzi kinachotolewa ni lazima kupanda miti.

"Kwasasa tupo kwenye mpango wa kuchimba visima ili kuhakikisha katika shule zote za msingi na sekondari zinahamasika kupanda miti na kutunza mazingira tunaanza hatua kwa hatua," alisema.

Mavunde alisema hatua hiyo inaunga mkono jitihada zinazofanywa na Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira za kutunza mazingira na kuifanya Dodoma kuwa ya kijani. Alisema: "Naishukuru serikali kwa kazi kubwa ambayo mmeendelea kuifanya ya kuhamasisha utunzaji wa mazingira Dodoma Mjini, kazi kubwa imefanyika chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais ya kuifanya Dodoma kuwa ya Kijani na sasa imeanza kuwa ya kijani".



Abiria wakilazimika kushuka kwenye daladala kabla kufika kwenye kituo cha Mbezi Luis, Dar es Salaam juzi, baada ya kuwApo foleni iliosababishwa na baadhi ya madereva wanaoshusha na kupakia abiria barabarani. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Wabunge wapigwa msasa Sheria ya Ununuzi wa Umma

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MAMLAKA ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) imetoa mafunzo kwa wabunge kuhusu umuhimu wa Sheria ya Ununuzi wa Umma Sura na. 410 ya Mwaka 2023 ambayo imepunguza mlolongo wa michakato ya manunuzi.

Mkurugenzi Mkuu wa PPRA, Dennis Simba, alitoa wasilisho hilo mwishoni mwa wiki, akisema moja ya faida za sheria hiyo ni kuweka upendeleo kwa kampuni za ndani.

Alisema zabuni zote zenye thamani hadi Sh.bilioni 50 zimetengwa kwa kampuni za ndani pekee.

"Kwa miradi mikubwa ya kimkakati sheria imetoa fursa kwa kampuni za ndani kuingia katika ushirika na kampuni za nje ambapo kampuni za ndani zitakuwa kiongozi wa ushirika huo," alisema.

Alisema sheria imeweka masharti ya kuepusha matumizi mabaya ya upendeleo huo. Simba alisema pia sheria imeweka sharti upendeleo kwa bidhaa zizotengenezwa, kuchimbwa au kazalishwa nchini hadi wa asilimia 15.

Vilevile, alisema sheria imeweka adhabu ya kinidhamu kwa mtumishi atakayenunua bidhaa, huduma au kazi za ujenzi kwa bei ya juu kuliko bei kikomo.

Kuhusu kuweka utaratibu wa ununuzi kwa taasisi za umma zinazojiendesha kibiashara alisema sheria imeweka masharti ya utaratibu wa ununuzi kwa taasisi za umma zinazojiendesha kibiashara

Alisema kanuni imeruhusu tamko la dhamana badala ya dhamana ya kibenki kwa zabuni zenye thamani hadi ya Sh. billioni 50

"Kanuni imeweka ukomo maalumu wa uidhinishaji kwa ofisa masuuli ili kupunguza mchakato wa ununuzi. Mathalani kuidhinisha mpaka wastani wa Sh. bil. 10 bila kuhitaji bodi ya zabuni kwa bidhaa, huduma na kazi za ujenzi" alisema

Mbunge wa Nyasa (CCM), Stellah Manyanya, alipongeza serikali kwa kuanzisha sheria hiyo na kuitaka mamlaka hiyo kumaliza changamoto za kimfumo ambazo bado zipo.

# Megawati 595 za umeme zakosa matumizi Singida

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

SHIRIKA la Umeme Tanzania (TANESCO) Mkoa wa Singida, limetoa wito kwa wawekezaji wa ndani na nje kuwekeza mkoani humo, kutokana na mkoa kuwa na ziada ya umeme wa megawati 595.96 ambao hautumiki kwa zaidi ya miaka miwili.

Ofisa Uhusiano na Huduma kwa Wateja TANESCO Mkoa wa Singida, Rehema Mwaipopo, alitoa rai hiyo jana kwenye mkutano wa wadau wa umeme ambao uliwashirikisha madiwani, viongozi wa CCM na watendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Singida.

Alisema katika kituo cha kupozea umeme kilichopo Kibaoni Manispaa ya Singida ambacho kimeunganishwa kwenye gridi ya taifa kina megawati 616 lakini matumizi ya Mkoa wa Singida ni wastani wa megawati 20.04 sawa na asilimia 3.3, hali inaoufanya mkoa kuwa na ziada ya megawati 595.69.

"Kuwa na ziada hii ya umeme maana yake ni kwamba katika mkoa wetu wa Singida tunahitaji wawekezaji wengi zaidi, kwa sababu tuna uwezo wa miundombinu ambayo ina uwezo mkubwa, hivyo tunahitaji watu wawekeze umeme huu utumike," alisema.

Msimamizi wa Miradi wa shirika hilo, Antony Msagwa, alisema kwa mwaka wa fedha 2024/2025 TANESCO Mkoa wa Singida imeanza kutekeleza miradi 16 kwa lengo kuboresha huduma, kusogeza miundombinu na kuunganisha wateja wapya 3,574.

Alisema Wizara ya Nishati kupitia TANESCO ina mpango wa kuongeza uzalishaji wa umeme kwa kuwa na vyanzo mbadala mkoani Singida ili kuwa na vituo viwili vya kuzalisha umeme kwa njia ya upepo na jua.

Alisema kituo cha umeme wa upepo kitajengwa Manispaa ya Singida na cha umeme wa jua kitajengwa wilayani Manyoni.

Msagwa alisema pamoja na mikakati inayofanywa na shirika kuhakikisha umeme unakuwepo muda wote, lakini kumekuwa na changamoto ya hujuma kwenye miundombinu ya zamani na mipya kutokana na wizi wa nyaya za shaba zinazotumika katika kuilinda mashine umba.

"Changamoto nyingine inayotukabili ni uwepo wa matukio ya moto kuunguza nguzo ambazo zimesimikwa kwenye miradi na maeneo ambayo huduma ya umeme inaendelea," alisema.

Kaimu Meneja wa TANESCO Mkoa wa Singia, Ernest Nyerere, aliwataka wananchi kuchukua tahadhari na kutoa taarifa wanapoona kuna changamoto ya miundombinu kama vile nguzo kuanguka au hitilafu ya umeme.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Singida, Ester Chaula, alilipongeza shirika hilo kwa maboresho makubwa ya utoaji huduma.

Baadhi ya madiwani wa halmashauri hiyo waliiahidi TANESCO kwamba watahakikisha wanahamasisha wawekezaji ili wajenge hata viwanda vidogo kwa kuwa uhakika wa umeme mkoani Singida ni asilimia 100.



# Waomba maboresho barabara Mbeya-Chunya kupunguza ajali

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKAZI wa Kitongoji cha Nsalaga katika Kata ya Lwanjilo Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wameiomba serikali kuiboresha barabara ya Mbeya-Chunya, ili kupunguza ajali ambazo zimekuwa zikitokea mara kwa mara na kusababisha vifo na ulemavu.

Wananchi hao ni wa eneo ilipotokea ajali ya basi la AN CLASSIC mwishoni mwa wiki na kusababisha vifo vya watu 12 na wengine 33 kujeruhiwa, ambapo wananchi hao wanadai kuwa ajali zimekuwa zikitokea kutokana na eneo hilo kuwa na mteremko na kona kali.

Balozi wa Kitongoji hicho, Isaka Mbuba alisema ajali zimekuwa zikitokea kila wiki katika eneo hilo na kusababisha madhara kwa wananchi, ambao baadhi wamekuwa wakipoteza maisha, wengine kuumia na hata vyombo vya usafiri kuharibika.

Alisema mteremko uliopo katika eneo hilo ni mkali na kuna kona ya ghafla ambayo imekuwa ikiwasumbua madereva wengi hasa ambao ni wageni na njia hiyo.

Alisema wakati barabara hiyo inajengwa, mkandarasi alianza kuchoronga upande wa pili ili kuiondoa kona hiyo, lakini baadaye akahama na kurejea kwenye njia hiyo ya zamani hali ambayo ilisababisha kona hiyo kuendelea kuwepo. "Hapa isipotokea ajali ya gari basi unakuta pikipiki, na hapa jana tu basi limeanguka hapa na kuua watu, tunaomba serikali ifanye utaratibu wa kuihamisha barabara hii ili kuiua kona hii maana vinginevyo watu wataendelea kufa," alisema Mbuba.

**"Hapa isipotokea ajali ya gari basi unakuta pikipiki, na hapa jana tu basi limeanguka hapa na kuua watu, tunaomba serikali ifanye utaratibu wa kuihamisha barabara hii ili kuiua kona...**

Taima Chisunga alisema pamoja na eneo hilo kuwa baya lakini hakuna alama yoyote ya tahadhari iliyowekwa ambayo inaonyesha kwamba kuna hatari na hivyo akaomba serikali iweke alama.

Alisema serikali kupitia Wakala wa Barabara nchini (TANROADS) inatakiwa kuweka matuta ambayo yatasaidia kupunguza mwendo wa magari kabla ya kufikia eneo hilo ambalo ni hatarishi.

Alisema mara nyingi wamekuwa wakishuhudia ajali ambazo zinakatisha maisha na kwamba baadhi ya wananchi wameanza kulihusisha eneo hilo na imani za kishirikina wakidai kuwa ajali zinatokea kwa sababu ya uchawi.

"Na sisi tumechoka kuona damu za watu zikimwagika, kila siku tunashuhudia Watanzania wenzetu wanakufa hapa, tunaomba serikali iweke miundombinu ambayo itatusaidia kupunguza ajali hizi," alisema Chisunga.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera aliagiza TANROADS kuweka bango linaloashiria kuwa eneo hilo kuna mteremko mkali na kona ili madereva waanze kuchukua tahadahri mapema.

Alisema mbali na eneo hilo pia maeneo mengine yote ya miinuko katika mkoa huo, inatakiwa kuwekewa tahadhari ambazo zitakuwa zinawasaidia madereva kuchukua tahadhari.

Hata hivyo aliwataka madereva wa magari ya abiria mkoani humo kuheshimu alama za barabarani kwa kuhakikisha wanazinga maelekezo ambayo alama hizo zinaelekeza.

Vilevile aliagiza Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani mkoani humo kudhibiti magari yote mabovu yanayobeba abiria mkoani humo ikiwa ni pamoja na kuyaondoa.



Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii ikikagua mradi wa ujenzi wa kituo cha utoaji taarifa kwa wageni wakati wa ziara ya kikazi ya kamati hiyo ya kukagua miradi iliyo chini ya ya Mradi wa Kuboresha Usimamizi wa Maliasili na Kukuza Utalii Kusini mwa Tanzania (REGROW) katika Hifadhi ya Taifa Ruaha, Mkoani Iringa. P**ICHA: MPIGAPICHA WETU.**

# Halmashauri Nyasa yavunja rekodi ukusanyaji mapato

**Na Gideon Mwakanosya,** NYASA

HALMASHAURI ya Wilaya ya Nyasa mkoani Ruvuma imevuka lengo la ukusanyaji mapato, baada ya kufanikiwa kukusanya Sh. bilioni 2.17 katika kipindi cha mwaka wa fedha 2023/2024.

Hayo yalisemwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Khalid Khalif kwenye kikao cha baraza la madiwani cha kujadili taarifa ya hesabu za mwisho kwa mwaka wa fedha za 2023/2024.

Alisema kuwa kati ya makusanyo hayo, mapato halisi ni Sh. bilioni 1.32 na mapato kutoka katika vyanzo zuiliwa ni zaidi ya Sh. milioni 859.

"Fedha za miradi ya maendeleo ambazo zimepokelewa katika kipindi hicho ni Sh.bilioni 11.8 ambazo zimetumika kwa ajili ya mfuko wa afya wa pamoja, elimu bure, TASAF, SEUIP, P4R, UNICEF, CDCF, chanjo ya polio, umaliziaji wa maboma, shule shikizi, BOOST na WASH," alisema Khalif.

Alibainisha kuwa mapato kutokana na kodi mbalimbali katika kipindi hicho yameongezeka kutoka Sh. milioni 202.3 kwa mwaka 2022/2023 hadi kufikia Sh. milioni 271.8 mwaka 2023/2024.

Mkuu wa Wilaya ya Nyasa, Peres Magiri aliagiza kufanyika vikao vya kamati ya afya ngazi ya wilaya ambavyo vinazungumzia suala la afya kwa ujumla ikiwemo kutambua suala la Virusi Vya Ukimwi (VVU) na vifo vya mama na mtoto.

Pia aliagiza ratiba ya vikao vya lishe ngazi ya halmashauri iandaliwe na kuhakikisha vikao vinafanyika kwa wakati, ili kutekeleza mikataba ya lishe katika ngazi zote hadi kata ili kukabiliana na udumavu.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa, Stewart Nombo aliwapongeza watumishi na madiwani kwa kusimamia ukusanyaji wa mapato.

# W'biashara, wakulima maparachichi kujengewa uwezo

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

CHUO cha Elimu ya Biashara (CBE) Kampasi ya Mbeya kimesema kinakusudia kuwakutanisha wafanyabiashara na wakulima wa maparachichi wa mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, ili kuwajengea uwezo wa kuchangamkia fursa za masoko ya kimataifa.

Mkutano huo unatarajiwa kufanyika kwa siku mbili mkoani Mbeya na kuhusisha pia maofisa mbalimbali wa serikali wakiwepo maofisa biashara ikiwa ni sehemu ya mikakati ya serikali kukuza sekta hiyo na kuongeza ajira kwa wananchi.

Mkurugenzi wa CBE kampasi ya Mbeya, Jeremiah Wilhelm aliyasema hayo mwishoni mwa wiki alipokuwa akitoa taarifa ya maendeleo ya chuo hicho ikiwemo uanzishaji wa kozi mpya na ujenzi wa miundombinu mipya.

Alisema mkutano huo unakusudiwa kufanyika hivi karibuni na kuhusisha zaidi ya makundi 50 ya wadau wa zao hilo ili kupanua wigo wa uelewa wa zao ilo pamoja na masoko ya kimataifa kwa lengo la kuinua uchumi wa wakulima na taifa.

"Zao hili ni miongoni mwa mazao ambayo yanaliingizia taifa fedha nyingi za kigeni kwa sasa kutokana na kwamba linauzwa kwa kiwango kikubwa nje ya nchi, kwahiyo tunataka kutumia utaalamu tulionao kuwaelimisha wadau wa zao hili," alisema Wilhelm. Alisema elimu hiyo inalenga pia kuboresha uzalishaji wa zao hilo ili kuwasaidia vijana kujiajili kupitia kilimo hicho hasa katika mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini ambayo hali yake ya hewa inavutia.

Kwa upande wake Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera aliupongeza uongozi wa chuo hicho kwa kuanzisha mpango huo akidai kuwa utasaidia serikali kufikia lengo la kuongeza uzalishaji wa zao hilo na kuongeza uwekezaji. Alisema wananchi wamekuwa wakijituma kwenye uzalishaji wa mazao mbalimbali lakini wanakosa elimu sahihi ya biashara hali ambayo inasababisha washindwe kuzalisha kwa kiwango kinachotakiwa.

"Wakulima wanalima na wafanyabiashara wanasafirisha mazao haya lakini tatizo lililopo ni kwamba hawazijui baadhi ya taratibu ikiwemo ubora wa mazao yanayotakiwa, kwahiyo naamini kwamba mkutano wenu utasaidia kutatua kero hizi," alisema Homera.

Hata hivyo alikipongeza chuo hicho kwa uwekezaji ambao kimefanya hasa kwenye ujenzi wa miundombinu mbalimbali ya kuwezesha wanafunzi na wahadhiri kufanya kazi vizuri.

Diwani Kata ya Iganzo, Daniel Mwaipopo alisema uwepo wa chuo hicho katika eneo lake umesaidia kuliamsha eneo hilo kimaendeleo kutokana na thamani ya ardhi yao kupanda.

Alisema baadhi ya wananchi wamejenga nyumba za kupangisha na wengine wameanzisha biashara ambazo zinapata soko kutokana na uwep wa wanafunzi.

# Serikali kuboresha mazingira huduma za maktaba

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla amesema serikali inaendelea kuchukua hatua madhubuti na haraka kwa kuweka mazingira bora ya huduma za maktaba.

Amesema lengo ni kuwarahisishia wanafunzi kujifunza pamoja na kutoa elimu iliyobora kwa wananchi wote wa Unguja na Pemba.

Aliyasema hayo jana katika kilele cha tamasha la vitabu na siku ya kisomo duniani lililofanyika katika Ukumbi wa Sheikh Idris Abdulwakil Kikwajuni Zanzibar.

Hemed alisema kuwepo kwa tamasha hilo kutasaidia kuenzi utamaduni wa kusoma, kuandika na kuhamasisha jamii kupenda kusoma vitabu kama njia mojawapo muhimu inayosaidia kufungua milango ya maarifa, ufahamu, ujasiri na kupata ustawi mzuri wa maendeleo.

Alisema serikali inaendelea na ujenzi wa maktaba kubwa na ya kisasa katika eneo la Maisara ambayo itatoa huduma kwa njia ya kidijitali itakayorahisisha huduma ya upatikanaji wa vitabu na kutanua wigo mpana wa usomaji wa vitabu kwa wananchi sambamba na kujenga maktaba nyingine sita kwa Unguja na Pemba.

Aidha alitaka Bodi ya Huduma za Maktaba Zanzibai kusogeza huduma zao kwa wananfunzi wa vyuo vya ufundi, vituo vya kulelea watoto yatima ili kujiendeleza na masomo yao pamoja na kujiongezea maarifa.

Hata hivyo aliwataka watendaji wa huduma za maktaba kuimarisha zaidi huduma za maktaba ili wananchi wengi kupata hamasa ya kujisomea pamoja na kujiongezea ujuzi utakaowasaidia katika maisha yao na jamii kwa ujumla.

Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Lela Mohamed Mussa alisema dhamira ya Dk. Mwinyi ya kuwekeza katika sekta ya elimu ni kuhakikisha anaondoa ujinga.

Mkurugenzi wa Bodi ya Huduma za Maktaba Zanzibar, Ulfat Abdulaziz Ibrahim alisema madhumuni ya kufanyika kwa tamasha la vitabu ni kuihamasisha jamii juu ya matumizi ya huduma za kimaktaba, kujenga tabia ya kusoma vitabu ambavyo vinawajengea uwelewa mpana jamii hasa wanafunzi wa shule.

Alisema maadhimisho hayo yanalenga kuielimisha jamii kuona umuhimu wa kusoma vitabu na kuwahimiza watoto kujenga tabia ya kwenda maktaba kujisomea, ili kuwaongezea maarifa na ujuzi kwa ustawi wa maisha yao.

Makamu Mkurugenzi wa mradi wa kusoma kutoka shirika la Room to read, Prisca Mdee alisema shirika hilo kwa kusaidiana na serikali inatekeleza mradi wa maktaba kwa kuazisha maktaba kwa shule za msingi.

Alisema hatua hiyo itasaidia kuendana na jitihada za kidunia ya mabadiliko ya kiulimwengu ambayo yapo kwenye mtandao, ambapo wanafunzi, wazazi, jamii, walimu na wadau kusoma vitabu na kupata taarifa kupitia teknolojia hiyo.

# Dk. Mwinyi: Zanzibar ina la kujifunza kutoka Indonesia

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk Hussein Ali Mwinyi amesema nchi ya Indonesia imepiga hatua kubwa katika masuala mbalimbali ikiwemo ya uchumi wa bluu, kwamba ina visiwa 17,000 hivyo Zanzibar inapaswa kujifunza kutoka nchi hiyo.

Alisema hayo juzi wakati akizungumza na waandishi wa habari katika Uwanja wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume, baada ya kurejea nchini akitokea Indonesia alikokuwa katika ziara ya kikazi.

Alisema katika biashara kuna fursa kubwa ya kuongeza biashara hasa katika masuala ya mwani, karafuu na uchumi wa bluu, uwekezaji na biashara.

Alisema nchi hiyo imepiga hatua kubwa sana katika sekta ya mafuta na gesi na inawasadia katika uchumi wao, hivyo aliwakaribisha Zanzibar kushirikiana katika kuchimba mafuta na gesi.

"Tayari tumeshafika hatua ya kukaribisha wawekezaji katika hatua hiyo, hivyo tumewakaribisha Indonesia kuja na kushirikiana na sisi katika eneo hilo" alisema. Akizungumzia kuhusu Bandari ya Mangapwani iliyopo Kaskazini Unguja, alisema serikali inania ya kupata wawekezaji ambapo itahitaji na sekta binafsi kushirikiana ili kwa pamoja kuwa na bandari jumuishi katika eneo hilo.

> **"Tayari tumeshafika hatua ya kukaribisha wawekezaji katika hatua hiyo, hivyo tumewakaribisha Indonesia kuja na kushirikiana na sisi katika eneo hilo" alisema.**

Aidha, alisema katika ziara hiyo ameshuhudia utiaji saini mkataba wa taasisi ya dawa na vifaa tiba ya Indonesia na Serikali ya Tanzania, ambapo serikali itanufaika katika masuala ya udhibiti wa dawa.

Dk. Mwinyi alisema nchi hiyo imeonyesha utayari wa kutoa nafasi za masomo ili vijana wa Zanzibar kwenda kujifunza nchini huko masuala ya dawa, hasa ikizingatiwa kuwa sekta ya utalii ni sekta mama kwa Zanzibar ikifuatiwa na sekta ya uchumi wa bluu.

Kuhusu mwani alisema Indonesia imepiga hatua kubwa katika zao hilo ambapo licha ya kuzalisha pia huchakata na kuongeza thamani, hivyo Zanzibar ni vyema ikajifunza kutoka katika nchi hiyo lakini pia masula ya uvuvi na uchumi wa bluu.

Alisema nchi hiyo inazalisha na kuchakata bidhaa ya karafuu ambapo alipata nafasi ya kutembelea kiwanda kinachotengeneza mafuta yanayotokana na majani ya karafuu.

Dk. Mwinyi alisema alikutana na mwenye kiwanda hicho ambapo alikubali kuisadia Zanzibar hasa ikizingatiwa kuwa inazalisha zao hilo na kuongeza thamani ya bei ya zao hilo.




Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla (wa pili kushoto) akiwa na Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja, Idrisa Kitwana (kulia kwa Makamu wa Rais) pamoja na Waziri wa Elimu, Lela Muhammed Mussa (kulia) wakisikiliza maelezo kutoka kwa Mkurugenzi Msaidizi wa mradi wa kusoma wa Shirika la kimataifa la Room to Read, Prisca Mdee baada ya kutembelea mabanda ya maonesho katika kilele cha tamasha la vitabu na siku ya kisomo duniani lililofanyika Kikwajuni Zanzibar juzi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Mkutano wa 16 Baraza la Wawakilishi kuanza kesho

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKUTANO wa 16 wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar unatarajiwa kuanza kesho, ambapo utakuwa na shughuli mbalimbali ikiwemo maswali na majibu 280.

Akizungumza na waandishi wa habari huko Chukwani Zanzibar kwenye ofisi za baraza hilo, Katibu wa Baraza, Raya Issa Msellem alisema pia kutakuwa na uwasilishwaji wa ripoti za wizara zote za serikali kuhusu utekelezaji wa maagizo ya kamati za kudumu za baraza hilo kwa mwaka wa 2023/2024.

Alisema katika mkutano huo pia kutawasilishwa mswaada mmoja uliosomwa kwa mara ya kwanza katika mkutano wa 15 ambapo utajadiliwa.

Akijibu maswali aliyoulizwa na waandishi wa habari kuhusu shughuli ya kiapo kwa mwakilishi mteule aliyeteuliwa hivi karibuni na Tume ya Uchaguzi Zanzibar ambae anajaza nafasi iliyoachwa wazi na mwakilishi wa Viti Maalum nafasi ya wanawake Mkoa wa Kusini Unguja, Panya Ali Abdallah aliyefariki dunia hivi karibuni, alisema bado baraza halijapokea jina la mteule huyo.

"Kama baraza bado hatujapokea jina la mteule huyo aliyeteuliwa na Tume ya Uchaguzi lakini jina lake litakapowasilishwa kwetu shughuli ya kumuapisha itafanyika hata kama kikao cha baraza kitakuwa kimeanza" alisema.

Aidha alisema kwa taratibu za baraza wajumbe wote wa kuteuliwa viti maalum pamoja na wanaochaguliwa majimboni huhalalishwa na Tume ya Uchaguzi na tume huandikia barua Baraza la Wawakilishi kuwasilisha majina yao.

"Tunasubiri jina kutoka Tume ya Uchaguzi na tutakapoletwa jina hilo tutaingiza katika ratiba ya kuapisha mteule huyo kwa sababu kanununi zinatutaka kama kuna mjumbe mpya anatakiwa kuingia barazani shughuli ya mwanzo lazima afanye kiapo" alisema.

Hivi karibuni Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC) kwa mamlaka iliyopewa chini ya Kifungu cha 55(3) cha Sheria ya Uchaguzi Namba 4 ya Mwaka 2018 imemtangaza Chumu Kombo Khamis kuwa mjumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa nafasi ya Viti Maalum vya wanawake kutoka CCM.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**GLADYS SEMSI** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0311/0052** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **FORODHANI SECONDARY SCHOOL** mwaka **1995.** Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. **Taarifa ya polisi: PHQ/DAR/KIN/191978/2024.**

## KUPOTEA KWA VYETI



**FROLA ADSON MWAILUNGA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S1873-0019** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **SONGWE SECONDARY SCHOOL** mwaka **2010.** Cheti cha Chuo chenye namba **734/CMLS/T/2014** kilichotolewa na **RUAHA UNIVERSITY (RUCU)** mwaka 2016. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/KIN/188869/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ERICK BRAYSON CHANAFI** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 485 DDF** aina ya **SUZUKI CARRY.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/NJO/WAN/3972/2024.**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**JUDICIARY**
**IN THE DISTRICT DELEGATED COURT OF MOROGORO**
**AT MOROGORO**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.53694 OF 2024**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE:**
**ALPHONCE JOHN PACHO-DECEASED**
**AND**
**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR A LETTER OF ADMINISTRATION BY BLANCA FLORENCE TEMBA........PETITIONER**

**GENERAL CITATION**
**(Made under rule 75 of the probate and administration of Estate rules, CAP352 R E 2019)**

ALL persons claiming to have any interest in the estate of the above- named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate(or letter of administration) is made to the above-named petitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the 27 day of 09, 2024.

Dated at Morogoro this 27 day of 08, 2024.

......................................
**Senior resident magistrate**
**MOROGORO**

## KUPOTEA KWA CHETI



**GWAMAKA ABDALLAH TWALIBU** Anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne (form four) chenye namba ya usajili **S05061-0048-2018** na namba ya checti ni CS18147291 kilichotolewa na shule ya **MONTFORT HIGH SCHOOL -RUJEWA MBEYA MWAKA 2018**, Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo cha polisi **PHQ/MBE/MBA/22605/2024.**

## KUPOTEA KWA VYETI




**MOSSES ENRICO EVARISTO** anatangaza kupoteza kwa vyeti vyake cha kumaliza kidato cha nne (4) chenye Index NO, S .3150 -0074 cha Shule ya Sekondari ya ILONGO cha mwaka 2010 .Cheti cha kumaliza kidato cha sita (6) chenye Index NO, S 0174 - 0521 cha Shule ya Sekondari ya CONSOLATA SEMINARY cha mwaka 2013 vilivyotolewa na BARAZA LA MITIHANI TANZANIA (NECTA) Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **IRI/IRI/RB/21303/2023.**

## KUPOTEA KWA VYETI



**SEIF YUSUPH RASHID** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S1770-0097** kilichotolewa na **IMAGE SECONDARY SCHOOL** mwaka **2013,** Cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S0123-0790** kilichotolewa na **KWIRO SECONDARY SCHOOL** mwaka 2016. cheti cha chuo chenye namba 2016/1574 kilichotolewa na **ST. JOHN'S UNIVERSITY OF TANZANIA** mwaka **2020.** Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. **TAARIFA YA POLISI: PHQ/DAR/KIN/191909/2024**

## KUPOTEA KWA CHETI



**CHRISTINA EDWARD MWITA** Anatangaza kupotea kwa cheti cha Stashada chenye registration namba NS.1877/0013/2019 kilichotolewa na wizara ya elimu maendeleo ya jamii, jinsia, wanawake na makundi maalum. chuo cha katati Mabhugai CDTTI Mwaka 2023 kwa yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi **.POLISI TAARIFA; PHQ/MAR/BUN/6131/2024.**

## KUPOTEA KWA VYETI



**JEREMIAH RICHARD LYAGULA** anatangaza kupotea vyeti cha kidato cha nne chenye index namba S.2464/0039/2015 kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **SONGAMBELE KILIMANI SECONDARY SCHOOL** Mwaka **2015** pamoja na Cheti Cha kidato Cha sita Chenye Index namba S.1093/0551/2018 kilichotolewa na Baraza la mitihani la Taifa(NECTA) kupitia **ALDERSGATE SECONDARY SCHOOL** Mwaka 2018, kwa yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. **POLISI TAARIFA; PHQ/MWA/NYA/33467/2024.**

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**TWAMBILILE JORDAN KAMOMONGA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA HATI YA KUSAFIRIA YENYE NAMBA **TAE294891** ILIYOTOLEWA NA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, HIVYO KWA YEYOTE ATAEFANIKIWA KUIONA HATI HIYO ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHOPO KARIBU NAE POLISI **TAARIFA DAR/URA/RB/65781/2022.**

OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.
MOB: +255 - 0677020701
E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.

## KUPOTEA KWA CHETI



**BERNARD DOTTO MAHEGA,** Anatangaza kupotolea na cheti cha darasa la saba chenye namba za usajili ps1306093-005 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia shule ya Nyamazugo Mwaka 2017. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo cha Polisi.
**TAARIFA YA POLISI: PHQ/DOD/DOD/25711/2024**

Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku
Piga Simu 0677020701

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

## Vifo vya kipindupindu Sudan vyafikia 185

**KHARTOUM,** Sudan

WIZARA ya Afya nchini Sudan imesema idadi ya vifo vinavyotokana na kipindupindu vimeongezeka kwa kiasi kikubwa hadi kufikia 185, huku vinavyotokana na mafuriko na mvua vikipanda hadi 205, na kuifanya idadi ya waliopoteza maisha kutokana na majanga hayo kufikia 390.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na wizara hiyo, baadhi ya visa vipya 268 vya kipindupindu vimerekodiwa, vikiwemo vifo 6 katika majimbo ya Kassala, Mto Nile, na Gedarif.

Ilisema hatua hiyo inasababisha jumla ya kesi za kipindupindu katika majimbo saba yaliyoathirika kufikia 5,692, ikiwa ni pamoja na vifo 185, na kwamba Agosti 12, mwaka huu mamlaka nchini humo ilitangaza kipindupindu kuwa janga la kitaifa.

Aidha, katika taarifa hiyo, Widhara ya Afya ilisema idadi ya waliofariki kutokana na mafuriko na mvua imefikia 205, huku wengine 886 wakijeruhiwa.

Hata hivyo, ilibainisha kwamba zaidi ya nyumba 26,000 zimeharibiwa kabisa, huku 33,000 zikiharibiwa kwa kiasi kutokana na mafuriko na mvua kubwa zinazoendelea kunyesha tangu Juni, mwaka huu.

Vile vile, siku chache zilizopita Shirika la Kimataifa la Uhamiaji (IOM) lilitangaza kuwa zaidi ya Wasudan 172,000 wamelazimika kuyahama makazi yao kutokana na mafuriko na mvua zinazonyesha katika majimbo 15 kati ya 18 tangu Juni. **TRT**

## 50 wafariki ajali ya lori Nigeria

**ABUJA,** Nigeria

TAKRIBAN watu 50 wamefariki kwa kuteketea na moto baada ya lori la mafuta kugongana na gari lingine lililokuwa limebeba wasafiri na Ng'ombe na kulipuka kaskazini mwa Nigeria.

Shirika la Usimamizi wa Dharura la Jimbo la Niger lilisema kuwa magari mengine kadhaa yalihusika katika ajali hiyo, iliyotokea jana.

Mkurugenzi Mkuu wa Usimamizi wa Dharura wa Jimbo la Niger, Abdullahi Baba-Arab, alionyesha hali ilivyokuwa baada ya ajali hiyo, akieleza kuwa waathiriwa walikuwa wamezikwa kwa wingi.

Gavana wa jimbo hilo Mohammed Bago aliwataka madereva kuchukua tahadhari na kuzingatia kanuni za barabarani ili kuzuia majanga hayo.

Kwa mujibu wa Kikosi cha Kitaifa cha Usalama Barabarani, ajali mbaya za barabarani zinazohusisha magari ya mafuta hutokea mara kwa mara nchini Nigeria, huku ajali 1,531 zikirekodiwa mwaka 2020 pekee, na kusababisha vifo vya watu 535 na wengine 1,142 kujeruhiwa,. **BBC**



Sudan inakabiliwa na mzozo wa kibinadamu unaozidi kuongezeka huku mafuriko na kipindupindu vikigharimu maisha ya mamia ya watu. **PICHA: AFP**

# Mgombea urais Venezuela akimbilia Uhispania

**CARACAS,** Venezuela

MGOMBEA wa upinzani kwenye uchaguzi wa rais nchini Venezuela Gonzalez, ameikimbia nchi yake kutokana na mzozo wa kisiasa na kidiplomasia kuhusu uchaguzi wenye utata uliofanyika Julai mwaka huu na kwenda Uhispania kuomba hifadhi.

Wizara ya Mambo ya Nje ya Uhispania ilisema katika taarifa jana, kwamba Gonzalez ni miongoni mwa walioppinga ushindi wa Rais Nicolas Maduro, na kwamba aliwasili kwenye kambi ya kijeshi ya Torrejon de Ardoz pamoja na mke wake.

Ilielezwa kuwa kuondoka kwa mwanasiasa huyo mwenye umri wa miaka 75 anayechukuliwa na Marekani, Umoja wa Ulaya (EU) na mataifa mengine ya eneo hilo kama mshindi wa uchaguzi, kunajiri wiki moja baada ya mamlaka za Venezuela kutoa hati ya kumkamata, zikimshutumu kupanga njama na uhalifu mwingine.

Mkuu wa Sera ya kigeni katika Umoja wa Ulaya Josep Borrell, alisema "Leo ni siku mbaya kwa demokrasia nchini Venezuela. Katika demokrasia, hakuna kiongozi wa kisiasa anayepaswa kulazimishwa kutafuta hifadhi katika nchi nyingine."

Makamu wa Rais wa Venezuela Delcy Rodriguez, alisema kupitia ukurasa wake wa mtandao wa Instagram kwamba mamlaka zilimpa njia salama Gonzalez kwa lengo la kurejesha amani ya kisiasa.

Ilielezwa kuwa baada ya kuondoka katika taifa hilo mwasiasa huyo alituma ujumbe kwa wafuasi wake akiwaarifu kwamba amelazimika kuondoka Venezuela kutokana na vitisho na ukandamizaji huku akiwahakikishia kwamba ataendelea kupambana kurejesha demokrasia nchini humo.

Upinzani nchini Venezuela ulisema matokeo ya uchaguzi wa Julai 28 yalimpatia ushindi Gonzalez na kwamba wamechapisha kwenye mtandao matokeo ya hesabu za kura wanazosisitiza zinaonesha ushindi wao.

Ilielezwa kuwa Rais Maduro aliyapinga madai hayo na kusema kulikuwa na njama kutoka kwa wanasiasa wa mrengo wa kulia kuihujumu serikali yake.

Uamuzi wa Gonzalez kuhamia Uhispania ni mtikisiko mwingine katika maisha ya mwanadiplomasia huyo wa zamani ambaye aliuacha ustaafu na kujitwika jukumu la kugombea urais wa Venezuela kwa tiketi ya upinzani mnamo mwezi Machi.

Ilielezwa kuwa amwanasiasa huyo alikubali kuchukua nafasi hiyo baada ya kiongozi wa upinzani Maria Corina Machado na mwanasiasa mwengine aliyeteuliwa na upinzani kugombea urais kuzuiwa kusimama kwenye uchaguzi huo.

**Ilielezwa kuwa kuondoka kwa mwanasiasa huyo mwenye umri wa miaka 75 anayechukuliwa na Marekani, Umoja wa Ulaya (EU) na mataifa mengine ya eneo hilo kama mshindi wa uchaguzi, kunajiri wiki moja baada ya mamlaka za Venezuela kutoa hati ya kumkamata, zikimshutumu kupanga njama na uhalifu mwingine.**

Machado aliandika kupitia ukurasa wake wa X kwamba Gonzalez yuko Uhispania na kwamba amelazimika kukimbia ili kulinda uhuru, uadilifu na maisha yake.

"Ongezeko la vitisho, miito polisi, hati za kukamatwa na hata majaribio ya kutaka kumlaghai na kumshinikiza awe mtiifu vinaonesha jinsi utawala ulivyokosa mipaka wala haya katika shauku yao ya kumnyamazisha na kujaribu kumvunja moyo," aliandika Machado.

Waziri wa mambo ya kigeni wa Uhispania Jose Manuel Albares alikiambia kituo kimoja cha televisheni nchini humo kwamba alimweleza Gonzalez kuwa „mtu yeyote anayetishiwa kushambuliwa kimwili au kuvunjiwa haki zake anakaribishwa Uhispania na kwenye balozi zake."

Alisema mipango ya kumruhusu kwenda Uhispania iliandaliwa kwa siku kadhaa na kwamba mchakato wa kumpatia hifadhi ya kisiasa unaanza mara moja.

Waziri wa mambo ya kigeni wa Uholanzi Caspar Veldkamp ameliambia bunge la nchi yake kuwa mwanzoni mwa mwezi Septemba, Gonzalez aliashiria dhamira yake ya kuondoka na kuendelea na mapambano yake nchini Uhispania.

Maofisa wa Uhispania ikiwemo Waziri Mkuu wa zamani Jose Luis Rodriguez Zapatero, aliyekuwa zamani na mahusiano mazuri ya kidiplomasia na Venezuela alihusika kwenye mazungumzo ya wiki nzima na watawala mjini Caracas ili zimruhusu Gonzalez kuondoka. **DW**

# TFF YAANIKA WACHEZAJI 10 WA KIKE WANAOCHEZA NJE

**Na Adam Fungamwango**

SHIRIKISHO la Mpira wa Miguu nchini (TFF), limesema mpaka sasa kuna wachezaji 10 wa kike wa Kitanzania wanaocheza soka la kulipwa nje ya nchi.

Ofisa Habari na Mawasiliano wa TFF, Cliford Ndimbo, akizungumza jijini Dar es Salaam jana, alisema hayo ni mafanikio makubwa kwa nchi katika mchezo wa soka hasa kwa kinamama ambao hauna muda mrefu sana, lakini tayari mafanikio yameanza kuonekana.

Alisema wanatarajia baada ya msimu huu wa mashindano kumalizika, wachezaji wengine wanaweza kuondoka nchini kwenda kucheza nje kwa kusajiliwa na klabu mbalimbali Afrika na Ulaya kwa ujumla.

Aliwataja wachezaji wa Kibongo wa kike wanaosakata kabumbu nje ya nchi mpaka sasa ni Ndela Patrick Luhala anayekipiga Klabu ya Tel Aviv University ya Israel, Nasnath Linus Ubamba na Suzana Adam Manumbu, wote wakichezea Klabu ya Tutankhamun FC ya Misri.

Wengine ni Maimuna Hamis Kaimu ambaye yupo anaitumikia FC Masr ya Misri, Julieth Singano anayekipiga FC Juarez ya Mexico, na Opa Clement anayesakata kabumbu katika Klabu ya Tukumbuke wa Henan ya China.

Wachezaji wengine wanaoipeperusha bendera ya Tanzania nje ya nchi, Ndimbo aliwataja kuwa ni Clara Cleitus Luvanga wa Al Nassr ya Saudi Arabia, Enekia Kasonga Lunyamila anayeichezea Mazatlan-femenil ya Mexico, Diana Lucas Msemwa wa Trabzonspor ya Uturuki na Aisha Khamis Masaka anayekipiga Ligi Kuu ya Wanawake England katika Klabu ya Brighton & Hove Albion.

## Azam FC yamuongezea mkataba Saadun

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Azam FC, imemuongeza mkataba mwingine wa mwaka mmoja Nassor Saadun baada ya kuridhishwa na kiwango chake.

Taarifa iliyotolewa na klabu hiyo jana imeeleza kuwa straika huyo sasa atasalia kwenye viunga vya Chamazi hadi 2026, huku kukiwa na uwezekano wa kuongezwa mkataba mwingine kama kiwango chake kitaendelea kuongezeka.

"Tumemuongeza mkataba wa mwaka mmoja straika wetu, Saadun na sasa ataendelea kuwapo Azam Complex, hadi 2026 akiendelea kututumikia," ilisema taarifa hiyo.

Azam ilimsajili mchezaji huyo mwanzoni mwa msimu huu akitokea Geita Gold ambayo imeshuka daraja kwa mkataba wa mwaka mmoja.

Straika huyo ni mmoja wa wachezaji waliocheza klabu nyingi nchini, ambapo mbali na Geita Gold amewahi kuzichezea Klabu za Fountain Gate, Singida United, Singida Big Stars, na Kagera Sugar.

Saadun ni zao la kikosi cha vijana chini ya miaka 17 cha Simba, ambapo alianzia wasifu wake kisoka kabla ya kupandishwa kwenye kikosi cha wakubwa 2017, lakini mwaka mmoja baadaye akatimkia Kagera Sugar.

Mchezaji huyo pia amecheza soka la kulipwa katika klabu mbalimbali nje ya nchi, kabla ya kurejea tena nchini kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara.






Jos Luis Mato Sanmartin maarufu Joselu, akishangilia sambamba na Lamine Yamal baada ya kuifungia timu yake bao kuongoza dhidi ya Switzerland kwenye mechi ya Kundi A ya Ligi ya Mataifa ya Ulaya, iliyopigwa juzi usiku katika Uwanja wa Stade de Geneve, Uswisi. **PICHA: MTANDAO**

## Kocha Mwembe Makumbi City alia na kiwango chao

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

LICHA ya kupata ushindi wa kwanza katika msimu wake wa kwanza kucheza Ligi Kuu Zanzibar, timu ya Mwembe Makumbi City, imesema hajaridhika na kiwango cha wachezaji wake katika mchezo huo.

Mwembe Makumbi City juzi iliibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya New City FC katika mchezo wa ligi hiyo uliochezwa Uwanja wa New Amaan Complex, visiwani hapa.

Akizungumza na Nipashe baada ya kumalizika mchezo huo, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Rajab Mrisho, alisema hajarishishwa na kiwango walichokionesha wachezaji wake katika mchezo wao huo wa kwanza.

Alisema walitengeneza nafasi nyingi za wazi, lakini washambuliaji wake walishindwa kuzitumia.

Mrisho alisema kwa kiwango walichoonesha si kama ni uwanagenzi wa ligi, lakini hawakuwa na maelewano mazuri katika uchezaji.

"Tumepata ushindi katika mchezo wetu wa kwanza, lakini ushindi huu nilitegemea kupata zaidi ya goli moja ila ndio hivyo pengine hii ndiyo ilikuwa ridhki yetu," alisema.

Naye Kocha Mkuu wa timu ya New City, Rashidi Lato, alisema kawaida mchezo wa kwanza unakuwa mgumu kutokana na timu zote kujiandaa vema.

Alisema alichokiona katika timu yake ni wachezaji wazamani na wapya kutokuwa na muunganiko mzuri hali iliyosababisha kushindwa kuzitumia nafasi walizotengeneza.

Hata hivyo, alisema wamejipanga kuyapatia ufumbuzi mambo ambayo wameyaona katika mchezo huo ili kuhakikisha mechi yao ya pili wanapata matokeo.

Ligi Kuu Zanzibar itaendelea tena leo, kukamilisha mzunguko wake wa kwanza ambapo utapigwa mchezo kati ya Malindi SC dhidi ya Zimamoto SC.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**VAN DIJK KUBAKI LIVER**

MKATABA wa nahodha wa Liverpool, Virgil van Dijk, unamalizika msimu ujao wa majira ya joto na mchezaji huyo wa Kimataifa wa Uholanzi mwenye umri wa miaka 33, amesema anataka kusaini mkataba mpya wa kusalia katika klabu hiyo hadi Kombe la Dunia la 2026. (*Mirror*)

**JORGINHO KUTORUHUSIWA**

ARSENAL haiko tayari kumruhusu kiungo wa kati wa Italia, Jorginho kuondoka katika klabu hiyo, licha ya kwamba Galatasaray inaripotiwa kutaka kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32, kabla ya dirisha la usajili la Uturuki kufungwa. (Talksport)

**TAH ALENGWA BARCELONA**

BARCELONA inamlenga mlinzi wa Bayer Leverkusen, Jonathan Tah mwenye umri wa miaka 28, na beki wa kulia wa Bayern Munich, Joshua Kimmich (29), ambao wote wanaichezea Ujerumani, huku kukiwa na sintofahamu kuhusu mustakabali wa beki wa Uruguay, Ronaldo Araujo mwenye umri wa miaka 25, na kiungo wa kati wa Uholanzi, Frenkie de Jong, 27. (*Mundo Deportivo*)

**PARTEY AGOMBEWA**

ATLETICO Madrid, Barcelona na Juventus ni miongoni mwa klabu zinazomtaka kiungo wa kati wa Ghana na Arsenal, Thomas Partey, 31. (*Caught Offside*)

**ENRIQUE MKATABA MPYA**

KLABU ya Paris St-Germain inashughulikia kuongeza mkataba wa kocha Luis Enrique, ambao kwa sasa unaendelea hadi Juni 2025. (*Fabrizio Romano*)

**DAVID KUFUNGWA TENA**

MSHAMBULIAJI wa Canada, Jonathan David, ambaye alihusishwa na Chelsea katika majira ya joto, amesema alifanya mazungumzo na „timu kadhaa" lakini alichagua kusalia Lille. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, aliongeza kuwa sasa anajadili kuongeza mkataba zaidi ya msimu ujao wa kiangazi na klabu hiyo ya Ufaransa. (*Athletic*)

**RABIOT AWINDWA UNITED**

KLABU ya Manchester United na Newcastle United zina nia ya kumsajili kiungo wa kati wa Ufaransa, Adrien Rabiot mwenye umri wa miaka 29, ambaye ni mchezaji huru baada ya kuondoka Juventus msimu wamajira ya joto. (*Caught Offside*)

**ASHWORTH AKERWA**

MKURUGENZI wa zamani wa michezo wa Newcastle United, Dan Ashworth, ambaye sasa yuko Manchester United, amekwazwa na shutuma kutoka kwa Paul Mitchell, mrithi wake katika Klabu ya St James' Park, ambaye amesema muundo wa klabu hiyo wa uhamisho "haufai kwa malengo" ya klabu. (*Telegraph*)

**KOSTIC HUYOOO FENERBAHCE**

KLABU ya Fenerbahce imekubali mkataba wa kumsaini winga wa Serbia, Filip Kostic mwenye umri wa miaka 31, kutoka Klabu ya Italia Juventus. (*Tuttosport*)

**DEPAY, CORINTHIANS SAFI**

FOWADI wa Uholanzi, Memphis Depay, ambaye ni mchezaji huru baada ya kuondoka Atletico Madrid, amekamilisha uchunguzi wa kimatibabu na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30, sasa anatazamiwa kusaini mkataba hadi 2026 na Klabu ya Corinthians ya Brazil. (*Fabrizio Romano*)

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# RODRYGO ASHANGAA KUACHWA BALLON D'OR

**MADRID,** Hispania

●●● Sitaki kuwadharau wachezaji waliopo, lakini nadhani nilikuwa na nafasi katika...

RODRYGO ameiambia ESPN kuwa „nimechukizwa" kwa kukosekana kwenye orodha fupi ya Ballon d'Or, baada ya kusaidia Real Madrid kushinda Ligi Kuu Hispania, LaLiga, na Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu uliopita.

**Wachezaji wenzake wa klabu Vinicius Junior, Jude Bellingham, Federico Valverde, Toni Kroos, Antonio Rudiger na Dani Carvajal waliteuliwa, pamoja na msajiliwa wa Madrid, Kylian Mbappe, lakini hakukuwa na nafasi kwa Rodrygo kwenye orodha ya wachezaji 30.**

"Nilikuwa na hasira, nadhani nilistahili," alisema Rodrygo akiiambia ESPN.

„Sitaki kuwadharau wachezaji waliopo, lakini nadhani nilikuwa na nafasi katika 30. Ilikuwa ni mshangao ... lakini hakuna mengi ninayoweza kufanya, si mimi ninayeamua mambo haya."

Mshindi wa Ballon d'Or atatangazwa katika hafla itakayofanyika Paris Oktoba 28, mwaka huu.

Rodrygo alifunga mabao 10 katika mechi 34 za LaLiga msimu uliopita, na pia kuzifumania nyavu mara tano kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Nafasi yake katika timu ya Madrid imekuja chini ya shinikizo kwa kuwasili kwa Mbappe, ingawa kocha Carlo Ancelotti ameendelea kumchagua kama sehemu ya safu ya wachezaji watatu hadi sasa katika kampeni hii.

Katika chapisho la hivi majuzi la mtandao wa kijamii, Rodrygo alichapisha msururu wa picha zake akinyanyua mataji akiwa na Madrid, zikiwa zimeambatana na emoji ya kucheka,.

"Niliandika chapisho la dhihaka," alisema Rodrygo. „Sasa hakuna mengi ya kusema. Kila mtu anajua hasira yangu. Kila mtu ameniunga mkono katika timu ya taifa na Real Madrid. Watu walituma ujumbe."

Rodrygo alikiri kwamba uwezo wake wa kufanya mambo mbalimbali umezuia maendeleo yake, hasa akiwa na Brazil, ambayo itacheza na Paraguay katika mechi ya kufuzu Kombe la Dunia Jumanne.

Fowadi huyo alifunga bao pekee katika mchezo huo katika ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Ecuador.

HABARI MICHEZO

# RONALDO APIGA BAO LAKE LA 901



**EDINBURGH,** Scotland

CRISTIANO Ronaldo alifunga bao la ushindi dakika za lala salama wakati timu yake ya Ureno ikishinda mabao 2-1 dhidi ya Scotland na kuendelea na mwanzo wao mzuri wa Ligi ya Mataifa ya Uefa.

Baada ya Bruno Fernandes kufunga bao la kusawazisha la Ureno, Ronaldo alifunga dakika ya 88 na kuwa bao lake la 901 katika maisha yake ya soka.

Scotland walipewa matumaini ya kupata ushindi wa kwanza dhidi ya Ureno tangu 1980 walipopata bao la kuongoza kupitia kwa Scott McTominay kwa kichwa dakika ya saba.

Lakini wageni hao walikosa la kuonesha kwa juhudi zao kwani Ronaldo mwenye umri wa miaka 39, aliitumikia tena nchi yake.

"Ushawishi huwa sawa, bila kujali kama anaanza kwenye benchi au la," alisema Fernandes, ambaye alicheza mchezo wake wa 600 kuhusu mchezaji mwenzake wa zamani wa Manchester United.

"Kila aliyeingia alileta tofauti. Cristiano ana bao, leo (juzi) amefunga bao la 901 na sasa yuko njiani kuelekea 1,000."

Ureno wanaongoza Kundi la 1 la Ligi A wakiwa na pointi sita baada ya kuanza kwa ushindi dhidi ya Croatia, walio nafasi ya pili kwa tatu kufuatia ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Poland Jumapili.

Scotland wamepata vipigo viwili, vyote kwa mabao ya dakika za lala salama. Walifika Lisbon wakiwa bado na uchungu baada ya kuchapwa mabao 3-2 nyumbani na Poland.

## Barcelona wapata pigo kwa Olmo

**BARCELONA,** Hispania

HISPANIA imemrejesha Barcelona Dani Olmo baada ya kupata jeraha la goti wakati wa sare ya bila kufungana na Serbia.

Mechi ya kwanza ya 'La Roja' hao yangu kutawazwa mabingwa wa Ulaya katika Euro 2024, iliisha bila bao, huku vijana wa Luis de la Fuente wakizuiliwa kwa suluhu ugenini mjini Belgrade Alhamisi usiku.

Mwishoni mwa kipindi cha pili, Olmo alilazimika kutolewa nje baada ya kuumia goti.

Kulikuwa na matumaini kwamba angeweza kupona kwa wakati kumenyana na Uswisi Jumapili, lakini sasa imeripotiwa kote kwamba mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26, atarejea Barca badala yake.

Ingawa jeraha hilo haliaminiki kuwa mbaya sana, iliamuliwa na Hispania kwamba itakuwa bora kwa Olmo kupumzika badala ya kuhatarisha majeraha zaidi.

Barcelona watarejea kwenye mechi ya LaLiga Jumapili ijayo watakaposafiri hadi kwa majirani zao wa Katalunya Girona, kabla ya kuanza kampeni ya Ligi ya Mabingwa Ulaya ugenini dhidi ya AS Monaco Alhamisi inayofuata.

Olmo ameanza vema maisha yake akiwa Barca, akifunga katika mechi zake mbili za kwanza - ushindi wa mabao 2-1 ugenini dhidi ya Rayo Vallecano ambapo alifunga bao la ushindi dakika za lala salama, na ushindi wa 7-0 dhidi ya Real Valladolid.

Barcelona wapo kileleni mwa jedwali baada ya misururu minne ya mechi.




# Van Dijk na mustakabali wake

**LIVERPOOL,** England

NAHODHA wa Liverpool na Uholanzi, Virgil van Dijk, amekiri kwamba alikuwa na hisia sana alipopendekeza maisha yake katika klabu na nchi yanaweza kumalizika.

Beki huyo alisisitiza kwamba 'atafikiria kwa makini' kuhusu mustakabali wake baada ya Uholanzi kushindwa kwa dakika za mwisho na England katika nusu fainali ya Euro 2024, ambayo ilikuja mara tu baada ya kupoteza mbio za kuwania taji la Ligi Kuu England akiwa na 'Wekundu' hao.

Julai mwaka huu, Van Dijk alisema: "Baada ya msimu kama huu, ambapo kila aina ya mambo yalifanyika na pia mashindano kama hayo na kila aina ya mambo yalifanyika, ambapo mimi mwenyewe pia nilitupwa kila aina ya mambo, basi hii inaumiza tu.

"Ninafanya kila kitu ili kushinda na kisha inakuwa na hisia mwishoni, kwa



sababu unajua yameisha. Sijui kwa sasa kuhusu mustakabali wangu. Nitafikiria kwa makini msimu huu wa majira ya joto kuhusu kile ninachotaka katika ngazi ya klabu na kama mchezaji."

Hata hivyo, baada ya ushindi wa Uholanzi wa mabao 5-2 dhidi ya Bosnia-Herzegovina Jumamosi usiku, Van Dijk aliwaambia waandishi wa habari kuwa ni 'mpiganaji' na amedhamiria kuongeza muda wake katika kiwango cha juu.

"Nilielewa kuwa haikuwa wazi jinsi nilivyohisi kuhusu hilo," alisema Van Dijk kuhusu maoni yake ya awali kuhusu mustakabali wake wa kimataifa.

"Bila shaka nilivunjika moyo sana baada ya mechi. Huenda ilionekana wakati huo kwamba ingekuwa mechi yangu ya mwisho ya kimataifa. Lakini mimi ni shujaa na mpiganaji na kamwe sitakata tamaa kwa ajili ya Oranje.

"Mwishowe, unapaswa kuangalia uwezo wako mwenyewe na kutathmini kama wewe bado ni muhimu vya kutosha. Hakika niko uwanjani na nje ya uwanja.

"Mimi ni nahodha wa Liverpool, jambo lisilobadilika na ninajihisi bora kimwili huku naendelea kuimarika kwenye mpira pia. Nataka kucheza Kombe lingine la Dunia. Najua bado nina ubora wa kutosha."

## HABARI MICHEZO

### Morocco aanika...

INATOKA UKURASA 24

tuliyoyaona, tuna uhakika wa kushinda,"alisema Morocco.

Naye Makamu wa Kwanza wa Rais wa TFF, Athuman Nyamlani, alisema wachezaji wako vizuri na wamezungumza nao, ambapo wamewaahidi kulipambania taifa kwa kucheza kwa juhudi zao zote kuhakikisha wanaibuka na ushindi.

"Wachezaji wetu wapo sawa, lakini kwenye soka matokeo yoyote yanaweza kutokea, hata hivyo tuna wachezaji ambao ni wazoefu kwenye michuano hii, kisaikolojia wapo sawa, hakuna aliyepata mshtuko eti kwa sababu tumepata sare nyumbani katika mchezo uliopita, tumekuwa tukizungumza nao na wametuhakikishia kufanya vizuri," alisema.

### Kagoma aishika...

INATOKA UKURASA 24

klabu," alisema Mwenyekiti huyo.

Alisema kuanzia leo ataanza kutoa taarifa rasmi kuhusu tukio hilo, lakini akasisitiza kuwa Kagoma hana kesi yoyote ya kujibu kwa sababu kila kitu kilikwenda kama kilivyopangwa.

"Kwa leo niishie hapa kwa sababu bado naendelea kupata vilelelezo, kesho nitaanza kutoa taarifa rasmi, ila naishia kusema hapaswi kumuomba mtu yeyote msamaha kwa sababu alikuwa mali ya klabu, ndiyo maana hata hao waliomfuata mchezaji walianza kuongea na klabu yake baada ya kupata baraka wakaenda kuongea na mchezaji.

"Sasa kama hakukuwa na maridhiano huwezi kusema mchezaji ambaye hakuwa wa kwako aombe msamaha, kwetu sisi tunaona ni kumdhalilisha mchezaji," alimaliza Mwenyekiti huyo wa SPUTANZA.

Inadaiwa kuwa Kagoma awali aliongea na Yanga, lakini baada ya kuchelewa kumtimizia mahitaji yake kwa muda ambao waliwekeana, alisaini Simba ambao waliilipa klabu yake na mchezaji mwenyewe, huku Fountain Gate pia ikitoa barua ya kumruhusu kujiunga na timu mpya.

Kwa sasa suala hilo lipo kwenye Kamati ya Sheria na Hadhi za Wachezaji huku akizuiwa kucheza mpaka litakapomalizika, licha ya kwamba alikuwa ameshacheza mechi moja ya Ligi Kuu.

# MAGOMA NA WENZAKE WASHINDWA RUFAA

**Na Grace Gurisha**

MZEE Juma Magoma ametoka Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam mikono nyuma huku akiwa ameshika chupa ya maji ya lita moja, baada ya rufaa aliyokata dhidi ya uamuzi mdogo uliyoipa ushindi Bodi ya Wadhamini wa Klabu ya Yanga kutupiliwa mbali.

Aidha, Magoma akiwa mbele ya Naibu Msajili wa Mahakama hiyo, Livini Lyakinana, muda wote alikuwa ameweka mikono yake kwenye mdomo wake na macho yake yakiwa yanamwangalia msajili huyo wakati anasoma hukumu hiyo hadi mwisho.

Akisoma uamuzi huo, Lyakinana kwa niaba ya Jaji Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Salma Maghimbi, aliyesikiliza rufaa hiyo, alisema uamuzi mdogo waliokuwa wanaupinga Magoma na wenzake haukatiwi rufaa.

"Uamuzi waliokuwa wanaupinga haukatiwi rufaa kwa mujibu wa sheria, rufaa inatupiliwa mbali," alisema Lyakinana wakati akisoma uamuzi huo kwa niaba ya jaji huyo.

Wakati wakiwasilisha hoja zao Wakili wa Yanga, Kalagho Rashid, aliwasilisha hoja za pingamizi la awali akipinga rufani iliyokatwa na wazee hao kwamba haipaswi kukatiwa rufaa kwa mujibu wa sheria.

"Haki za msingi za wadaawa ziliamuliwa katika shauri la marejeo ambalo pande zote mbili zilisikilizwa na wadaawa waliwakilishwa na mawakili wao, hivyo uamuzi huo haupaswi kukatiwa rufani," alidai Wakili Rashid

Alidai kuwa rufaa hiyo imeshapitwa na tukio kwa kuwa tayari Mahakama ya Kisutu imeshasikiliza maombi yao ya marejeo na kutengua hukumu yake ya awali hivyo hakuna chochote kinachoweza kubadilishwa hata kama rufaa yao ikikubaliwa.

Akijibu hoja hizo, Wakili wa Magoma, Jacob Mashenene, alidai uamuzi uliotolewa na Mahakama ya Kisutu unaamua haki za msingi za wadaawa kwa sababu hakuna shauri lolote lililobaki mahakamani baada ya uamuzi uliotolewa.

Wakili Mashenene alidai kuwa hoja ya rufaa hiyo imepitwa na wakati, alidai kuwa hoja hiyo haifai kuwa hoja ya pingamizi kwa sababu mahakama itatakiwa kutafuta ushahidi kuthibitisha hilo.

"Naomba mahakama itupilie mbali pingamizi la awali lililowasilishwa na Bodi ya Wadhamini Yanga na rufaa yao iendelee kusikilizwa,"alidai Mashenene

Magoma na mwenzake wanapinga uamuzi wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu uliokubali ombi lao la bodi hiyo kufungua nje ya muda maombi ya marejeo ya hukumu iliyobatilisha Katiba ya Klabu hiyo ya mwaka 2010.

Aidha, Magoma na mwenzake wamekata rufaa hiyo dhidi ya Bodi ya Wadhamini wa Klabu ya Yanga, ambayo ndio mjibu rufaa wa kwanza.

Wajibu rufaa wengine ni waliowahi kuwa wajumbe wa Bodi ya Wadhamini wa Klabu hiyo, Fatma Abeid Karume ( bado mjumbe mpaka sasa), Abeid Abeid na Jabiri Katundu (mjibu rufaa wa pili, wa tatu na wa nne mtawalia).

Wamekata rufaa hiyo wakipinga uamuzi huo wa Mahakama ya Kisutu kwa madai kuwa iliwapa wadhamini hao wa Yanga ruhusa ya kufungua maombi hayo ya marejeo ya hukumu hiyo bila wao kupewa nafasi ya kusikilizwa katika maombi hayo ya Yanga.

### MAGONGO...




Wanafunzi wa Shule za Msingi Kiwalani na Majani ya Chai, wakifanya mazoezi ya mpira wa Magongo katika Uwanja wa Kituo cha Michezo cha Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Coastal yawahi Dar kuikaribisha Mashujaa FC

**Na Shufaa Lyimo**

KIKOSI cha Coastal Union leo kinatarajia kutua jijini Dar es Salaam kwa ajili ya kujiandaa na mchezo wao ujao dhidi ya Mashujaa FC utakaopigwa Septemba 13, mwaka huu, katika Uwanja wa KMC uliopo Mwenge, Dar es Salaam.

Akizungumza na Nipashe jana, Msemaji wa timu hiyo, Abbas el Sabri, alisema wachezaji wote wana morali ya juu kuelekea katika mchezo huo ambao unatarajiwa kuwa mgumu na wenye upinzani mkubwa.

"Kesho (leo), tutaanza safari kuelekea Dar es Salaam kwa ajili ya kujiandaa na mchezo wetu dhidi ya Mashujaa, ambao tutaucheza kwenye Uwanja wa KMC, Dar es Salaam, alisema El Sabri.

Alisema wachezaji wote kiafya wanaendelea vizuri na kudai mpaka sasa hakuna mchezaji yeyote ambaye ni majeruhi.

Aidha, alisema mchezaji wao Lameck Lawi, kwa sasa yupo tayari kucheza na kuweka wazi ataonekana siku hiyo katika mchezo huo.

Aidha, alisema kuwa kwa sasa mchakato wa kumtafuta kocha mkuu bado unaendelea na kwamba zoezi hilo likikamilika watawafahamisha Watanzania wajue kinachoendelea.

"Mchakato wa kutafuta Kocha Mkuu unaendelea vizuri, tukimpata pamoja na wasaidizi wake tutatoa taarifa kwa mashabiki wetu," alisema msemaji huyo.

# Michezo

Nipashe


Jumanne Septemba 10, 2024




**Rodrygo ashangaa kuachwa Ballon d'Or** UKURASA 21

## CHUMA HICHO...!





Cristiano Ronaldo akiifungia timu yake ya Ureno bao la ushindi wakati ikishinda 2-1 dhidi ya Scotland kwenye mechi ya Kundi 1 ya Ligi ya Mataifa ya Ulaya iliyopigwa juzi katika Uwanja wa Estadio da Luz, Ureno. **PICHA: MTANDAO**

# Morocco aanika mbinu Stars kuiua Guinea leo

## ●●● Asema wanachotaka ni ushindi tu, wachezaji morali juu wataka kupata...

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Taifa ya soka ya Tanzania, Taifa Stars, leo itashuka kwenye Uwanja wa Charles Konan Banyo, uliopo mjini Yamoussoukro nchini Ivory Coast kucheza mchezo wa pili wa Kundi H, katika kampeni yake ya kusaka tiketi ya kucheza fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON) mwakani nchini Morocco, dhidi ya Guinea.

Mechi hiyo itakayopigwa saa 1:00 usiku kwa saa za Tanzania, inachezwa nchini humo kutokana na nchi ya Guinea kutokuwa na viwanja vinavyokidhi viwango vilivyowekwa na Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika (CAF) kwa ajili ya mechi za kimataifa inazozisimamia.

Mchezo huo unachezwa siku sita tu baada ya Stars kulazimishwa suluhu nyumbani, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam dhidi ya Timu ya Taifa, Ethiopia.

Stars inacheza na timu ambayo katika mchezo wa kwanza ilipata kipigo cha bao 1-0 dhidi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, ikiwa ugenini.

Kaimu Kocha Mkuu wa timu hiyo, Hemed Suleiman ‚Morocco', amesema kikosi chake kiko tayari kwa mchezo huo na hakina majeruhi yeyote, huku akisisitiza kuwa mchezo wa leo wataingia na mbinu tofauti na walivyocheza Dar es Salaam, kwani watashambulia zaidi ili kupata pointi tatu ambazo zitawafanya kukaa sawa kwenye msimamo wa kundi hilo.

"Vijana wetu wapo tayari, tunajua mechi hii ni ngumu, haya ni mashindano ya kufuzu AFCON, kila timu inajitahidi ili ifuzu na nchi zao pia wamezipa umuhimu mkubwa, lakini tutapambana.

"Wenzetu hawa walianza vibaya mechi ya kwanza, walifungwa bao 1-0 na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, sisi hatukufanya vibaya sana tumetoka suluhu, kwa hiyo malengo yetu ni kushinda mechi hii," alisema Morocco.

Kocha huyo ametaja mfumo na mbinu atakayotumia kwenye mchezo wa leo kuwa ni wa kushambulia zaidi

"Tutashambulia zaidi, huo ndiyo mfumo tutakaotumia, kwa sababu hakuna kingine tena, tunahitaji pointi tatu. Mpira siku hizi unachezwa popote pale, kwa jinsi tulivyocheza mechi iliyopita kipindi cha pili na tumerekebisha na makosa

INAENDELEA UK. 23

## Kagoma aishika pabaya Yanga

**Na Adam Fungamwango**

MWENYEKITI wa Chama cha Wachezaji wa Mpira wa Miguu Tanzania, (SPUTANZA), Mussa Kisoki, ameibuka na kusema mchezaji Yusuph Kagoma hapaswi kumuomba msamaha mtu au klabu yoyote kwa kilichotokea na kufanya hivyo ni kumdhalilisha.

Kisoki alisema hayo kutokana na Klabu ya Yanga, kupitia kwa Ofisa Habari wake, Ali Kamwe, kumtaka mchezaji huyo kuomba msamaha kwa alichowafanyia ili wamruhusu kuichezea klabu yake ya sasa, Simba.

Yanga imepeleka shauri kwenye Kamati ya Sheria na Hadhi za Wachezaji juu ya mchezaji huyo kuwa alichukua pesa zao na kusaini mkataba, lakini baadaye wakasikia amesaini tena kwenye Klabu ya Simba.

Hata hivyo, Kamwe alidai ili wamwachie wanataka mchezaji huyo aombe radhi, la sivyo watamhesabu kama ni mchezaji ambaye amesaini pande mbili.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Kisoki alisema kwa jinsi alivyolishughulikia suala hilo tangu Ijumaa iliyopita na vielelezo alivyoletewa, Kagoma hapaswi kumuomba mtu au klabu yoyote msamaha na yeyote anayetaka hivyo, basi nia yake ni kumdhalilisha mchezaji.

"Tumeanza kulishughulikia suala la Kagoma tangu Ijumaa na tumepata vielelezo vinavyoonesha suala hili halikuhitajika liwe la muda mrefu kiasi hiki, lilitakiwa limalizike tangu huko nyuma, lakini kuna watu wanataka kutunishiana misuli tu kwa ajili ya mchezaji.

"Kagoma alikuwa mchezaji wa Fountain Gate sasa ukienda kwenye kanuni za shirikisho zinazoongoza ligi, kuna kanuni ya 59 ya uhamisho ambayo yeye anaingia hapo, haingii kama mchezaji anayemaliza mkataba wake, au yupo huru anatoka kwenye klabu, anaamrishwa na klabu nini cha kufanya, hakuna kosa lolote alilofanya Kagoma, kila alilokuwa akifanya ni kwa maelekezo ya

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >